JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA (ACSEE), 2020

## 121 KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA

# (ACSEE), 2020

# 121 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI. ........ iv
1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA ........ 3
2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI ........ 3
2.2 SEHEMU A ........ 3
2.2.1 Swali la 1: Ufahamu ........ 3
2.2.2 Swali la 2: Utumizi wa Lugha ........ 7
2.2.3 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi ........ 11
2.2.4: Swali la 4: Matumizi ya Sarufi ........ 14
2.3.2 Swali la 5: Utungaji ........ 18
2.3.3 Swali la 6: Maendeleo ya Kiswahili ........ 20
2.3.4 Swali la 7: Maendeleo ya Kiswahili ........ 24
2.3.5 Swali la 8: Tafsiri na Ukalimani ........ 30
3.0 SEHEMU YA II: MTIHANI WA KISWAHILI KARATASI YA PILI. ........ 36
3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI ........ 36
3.2 SEHEMU A ........ 36
3.2.1 Swali la 1: Fasihi Kwa Ujumla ........ 36
3.2.2 Swali la 2: Maendeleo ya Fasihi Simulizi ........ 39
3.2.3 Swali la 3: Maendeleo ya Fasihi Simulizi ........ 43
3.3.2 Swali la 4: Usanifu wa Maandishi ........ 45
3.3 SEHEMU B ........ 50
3.3.1 Swali la 5: Uhakiki wa Ushairi ........ 50
3.3.2 Swali la 6: Uhakiki wa Ushairi ........ 55
3.3.3 SWALI LA 7 UHAKIKI WA RIWAYA ........ 59
3.3.4 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya ........ 63
4.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA ........ 67
5.0 HITIMISHO ........ 68
6.0 MAONI NA MAPENDEKEZO ........ 69
KIAMBATISHO A ........ 70
KIAMBATISHO B ........ 71

# DIBAJI

Taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Kidato cha Sita 2020 katika somo la Kiswahili imeandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania. Taarifa hii inalenga kutoa mrejesho wa ufaulu wa wanafunzi, walimu, wazazi, watunga sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Mrejesho wa ufaulu ni tathmini ya mwisho yenye azma ya kuonesha namna mfumo wa elimu nchini uliyofanikiwa kutoa elimu kwa ujumla hususan katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Vilevile, majibu ya watahiniwa katika mtihani huu yanalenga kuonesha namna mfumo wa elimu ulivyofanikiwa au ulivyoshindwa kuwapa maarifa watahiniwa wa Kidato cha Sita.

Uchambuzi wa sababu mbalimbali zilizochangia watahiniwa kujibu vizuri, wastani au vibaya maswali ya mtihani huu zimeainishwa. Sababu za baadhi ya watahiniwa kutojibu maswali kwa usahihi ni pamoja na kushindwa kutambua matakwa ya swali na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali katika somo la Kiswahili. Aidha, uchambuzi huu umeonesha sababu za watahiniwa kujibu maswali kwa usahihi kama vile: kutambua matakwa ya swali, kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa na kuzingatia kanuni na matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Pia, sababu za watahiniwa kupata alama za wastani zimebainishwa haswa katika kutoa majibu yasiyojitosheleza. Sababu hizi na nyinginezo zilizoainishwa katika taarifa hii zitawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa shule, walimu na wanafunzi kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu katika mitihani ijayo.

Baraza la Mitihani la Tanzania liko tayari kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na umma kwa ujumla ambayo yatatumika kuboresha taarifa za uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika siku za usoni.

Mwisho, Baraza linapenda kuwashukuru maafisa mitihani, walimu wa somo na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii. Shukrani za pekee ziwaendee wafanyakazi wa Kurugenzi ya Utafiti, Tathmini na Huduma za Kompyuta walioshiriki katika uchambuzi wa data zilizotumika katika taarifa hii.



Dr. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kidato cha sita ulianza kufanyika mwishoni mwa mwezi Juni mpaka katikati mwa mwezi Julai 2020. Mtihani wa somo la Kiswahili ulifanyika mwanzoni mwa mwezi Julai. Maandalizi ya mtihani huu yalizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili wa Kidato cha V na VI. Somo hili lilikuwa na karatasi mbili (2) za mtihani ambazo ni 121/1 Kiswahili 1 na 121/2 Kiswahili 2.

Mtihani wa 121/1 Kiswahili 1 ulikuwa na sehemu mbili (2), A na B. Mada zilizotahiniwa katika mtihani huu ni pamoja na Ufahamu na Ufupisho, Utumizi wa Lugha, Matumizi ya Sarufi, Utungaji, Maendeleo ya Kiswahili na Tafsiri na Ukalimani. Sehemu A ilikuwa na alama arobaini (40). Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote manne (4). Sehemu B ilikuwa na maswali manne (4) na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu (3) tu. Kati ya maswali hayo, swali la nane (8) lilikuwa la lazima na sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama sitini (60).

Mtihani wa 121/2 Kiswahili 2 ulikuwa na sehemu mbili (2), A na B. Mtihani huu ulitahini mada za Fasihi kwa Ujumla, Maendeleo ya Fasihi Simulizi, Usanifu wa Maandishi na Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi. Sehemu A ilikuwa na alama arobaini (40) na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali manne (4), mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu (3) na swali la tano lilikuwa la lazima. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama sitini (60).

Jumla ya watahiniwa 20,784 walifanya mtihani wa 121 Kiswahili, kati yao wasichana walikuwa 10,958 na wavulana walikuwa 9,826. Watahiniwa wote waliofanya mtihani huu walipata wastani wa alama 35, hivyo, ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili kwa mwaka 2020 kulikuwa kwa kiwango cha asilimia 100. Watahiniwa walifaulu katika viwango vitatu yaani vizuri kuanzia alama 60 hadi 100, wastani kuanzia alama 35 hadi 59 na hafifu kuanzia alama 0 hadi 34. Aidha, chati za viwango vya ufaulu kiasilimia zimeambatanishwa mwishoni mwa taarifa hii. Ufaulu wa watahiniwa umefafanuliwa kwa kutumia rangi tatu, rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.

Taarifa hii imejikita katika uchambuzi wa maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu. Lengo la uchambuzi huu ni kuonesha hali halisi ya jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika karatasi ya kwanza (121/1) na karatasi ya pili (121/2) ya mtihani wa somo la Kiswahili. Uchambuzi unaonesha kilichotarajiwa kufanyika na kilichofanywa na watahiniwa. Aidha, sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa kama vielelezo vya majibu halisi ya watahiniwa.

Kwa kupitia uchambuzi huu wadau mbalimbali wanashauriwa kutumia taarifa hii ili kuweka mpango mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili katika mada husika, hususan zenye ufaulu usioridhisha na kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

## 2.0 SEHEMU YA I: KISWAHILI KARATASI YA KWANZA

## 2.1 TATHMINI KWA KILA SWALI

## 2.2 SEHEMU A

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne, mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote na kila swali lilikuwa na alama kumi (10).


### 2.2.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali hili lilikuwa la Ufahamu, watahiniwa walitakiwa kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali waliyopewa.

Swali hili lilitoka katika mada ndogo ya dhana ya *Ufahamu* na lilikuwa mahsusi katika kupima ufahamu wa mtahiniwa katika kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yaliyohusiana na habari waliyosoma. Swali hili lilikuwa na vipengele vinne, (a) hadi (d).

Kipengele (a) katika swali hili, kilimtaka mtahiniwa kuandika kichwa cha habari aliyosoma. Katika kipengele (b) Mtahiniwa alitakiwa kueleza maana za maneno aliyopewa; (i) Zilifana (ii) Majilio (iii) Kutamalaki na (iv) Utandawazi kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Kipengele (c) mtahiniwa alitakiwa kutaja manufaa matatu ya sanaa za maonesho na kipengele (d) kilimtaka mtahiniwa kufafanua kauli aliyopewa.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 20,781. Watahiniwa wengi (99.6) walijibu vizuri swali hili na ufaulu wao ulikuwa wa wastani na zaidi kutokana na kutoa majibu sahihi katika vipengele vingi. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 1**: *Ufaulu wa Watahiniwa Kiasilimia*

Watahiniwa 19,015 sawa na asilimia 91.5 walipata alama za juu kuanzia 6 hadi 10. Ufaulu huu unaonesha kuwa, watahiniwa walikisoma na walikielewa vyema kifungu cha habari na kuweza kujibu vipengele vingi kwa usahihi. Kati yao, watahiniwa asilimia 45.2 walipata alama za juu zaidi kuanzia 8 hadi 10 kwa kuwa waliweza kuandika kwa usahihi kichwa cha habari, kutoa maana za maneno kama yalivyotumika katika habari, kutaja manufaa matatu ya sanaa za maonesho na kufafanua kauli waliyopewa. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliweza kujibu kipengele *(a) SANAA ZA MAONYESHO,* (b) alieleza maana ya maneno aliyopewa kama yalivyotumika katika habari *(i) zilifana – zilipendeza ama zilikuwa nzuri, (ii) majilio – kuwa na ujio au kuja,(iii) kutamalaki – kutawala, (iv) utandawazi – ni hali ya dunia nzima kuwasiliana kwa urahisi.* Pia alitoa majibu sahihi katika kipengele (c) na (d). Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kwa kujibu kwa usahihi vipengele (a), (b), (c) na (d).

01. (a) SANAA ZA MAONYESHO

(b) i) Zilifana
Neno zilifana kama zilivyotumika kwenye habari hiyo ina maana ya kuwa zilipendeza ama zilikuwa nzuri

ii) Majilio
Majilio kama jinsi ambavyo limetumika kwenye habari hii lina maana ya kuwa ni ujio au kuja

iii) Kutamalaki
Neno hili kama lilivyotumika kwenye habari lina maana ya kutawala.

iv) Utandawazi
Kama lilivyotumika kwenye habari hiyo neno hilo utandawazi lina maana ya ile hali ya dunia nzima kuwa kama kitu kimoja

c) Manufaa ya Sanaa za Maonesho

i) Sanaa za Maonesho zina kuza utamaduni wa jamii husika.

ii) Sanaa za Maonesho huwa kutanisha

01. (c) - Watu au Kuwaunganisha

iii) Sanaa za Maonyesho ina tambuli sha Jamii


(d) Mwandishi anaposema "Sanaa za Maonyesho zilifanya kazi ya mwalimu na mwanafunzi katika darasa maalumu ana maana ya kuwa Sanaa za maonyesho zililenga katika kuwakuza vijana wawe na maadili mema na kuwaandaa kushiriki majukumu mbalimbali na kuwa na Uzalendo pamoja na Ushujaa na kuwa raia wema wa siku zijazo.

**Kielelezo Na. 1.1**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kwa ufasaha.

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa, watahiniwa 1,674 sawa na asilimia 8.1 walipata alama kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kutoa majibu yasiyokidhi matakwa ya swali kwa baadhi ya vipengele. Kwa ujumla, ufaulu huu ulikuwa wa wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu sahihi katika kipengele (a) aliandika vizuri kichwa cha habari "*SANAA ZA MAONESHO",* lakini akatoa majibu yasiyo sahihi katika vipengele (b) alishidwa kueleza maana ya baadhi ya maneno aliyopewa (i) alitoa maana ya neno *"zilifana"* ambayo haikuwa sahihi kwa kueleza maana yake kuwa ni *kuwiana sawasawa*, (iii*) "kutamalaki" akitoa maana kuwa ni kusambaa* katika kipengele (d) alishindwa kufafanua kauli ya mwandishi kwa usahihi hivyo, alipata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa 92 sawa na asilimia 0.4 walipata alama za chini kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kutokuelewa kifungu cha habari na hivyo kushindwa kujibu vipengele vingi vya maswali yaliyoulizwa. Watahiniwa wengine walielezea maana za maneno bila kuzingatia muktadha wa neno katika kifungu cha habari na wengi wao walishindwa kuandika kichwa cha habari kilicho sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kujibu kwa usahihi katika vipengele (a) aliandika kichwa cha habari kuwa ni "*UTAMADUNI WA AFRIKA*" (b) (i) alitoa maana ya "zilifana" kuwa ni *zilizofurahisha utamaduni wa kiafika* badala ya *tenda kitu kwa namna*

*nzuri/kuridhisha/kushamiri* na (iii) kutamalaki alijibu kuwa ni *kuonekana* badala ya *kutawala/miliki/kustawi* (c) mtahiniwa aliyetaja kimakosa *matambiko, michezo ya watoto* na *mivigha* kama manufaa matatu ya sanaa za maonesho (d) alishindwa kufafanua kauli aliyopewa. Kielelezo Na. 1.3 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini.


6 (a) UTAMADUNI WA AFRIKA

(B) (i). Zilifurahisha na kuburudisha utamaduni wa kiafrika.

(ii) Ujio au kuja kwa wakoloni nchini Afrika.

(iii) Kuonekana.

(iv) Umoja na mshikamano.

(C) i/ Matambiko

ii/ Michezo ya watoto

iii/ Mivigha.

(D) Mwaandishi anamanisha kwamba sanaa za maonyesho zilikuwa zina funzo kuhusu kupata mtaala maalumu darasani kama elimu ya leo inavyotolewa ijapo kwa sanaa ya maonyesho ilikuwa ni elimu za kijamii kama vile jando and unyago,


**Kielelezo Na 1.2**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu kinyume na matakwa ya swali

### 2.2.2 Swali la 2: Utumizi wa Lugha

Swali lilitoka katika mada ya *Utumizi wa Lugha* katika kipengele cha *rejesta* na lililenga kupima Matumizi. Swali liligawanyika katika vipengele viwili, kipengele (a) kilimtaka mtahiniwa kufasili neno rejesta na kipengele (b) kilimtaka mtahiniwa kufafanua matumizi manne ya rejesta, swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 20,778 sawa na asilimia 99.9 ya watahiniwa waliofanya mtihani na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri sana. Asilimia 95 ya waliofanya swali hili walifaulu kwa

kiwango kizuri na kile cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 2**: *Ufaulu wa Watahiniwa Kiasilimia*

Watahiniwa 17,894 sawa na asilimia 86.1 walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Kati yao, asilimia 53.7 walipata alama za juu kuanzia alama 8 hadi 10 kwa kuwa, waliweza kutumia maarifa stahiki katika kufafanua matumizi ya rejesta kama vile*: kutambulisha wazungumzaji kuwa ni wa kundi fulani*, *kutumika kuficha ujumbe kwa watu wasio husika*, *husaidia kukuza lugha na kuweza kukidhi haja ya mawasiliano*. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kufasili rejesta na kufafanua matumizi yake.

2. A. Rejesta

Ni mtindo wa lugha unaotumika katika mazingira maalumu yenye shughuli fulani. Mtindo huu huzingatia matumizi ya maneno yanayoendana na mazingira husika. Mfano wa Rejesta ni kama; Rejesta za kanisani.
Rejesta za msikitini.
Rejesta za shuleni.
Rejesta za mgahawani


Mfano: 1

Nani chai kuku
Hii ni rejesta ya Mgahawani au hotelini kati ya mhudumu na mteja.

Mfano. 2.

Tumsifu yesu kristu.
Hii ni rejesta ya kanisani kati ya mchungaji na waumini

B. (i) Rejesta hutumika kuokoa muda.
Mfano: Rejesta za Mgahawani na hospitalini.
:Mhudumu; Nani wali mbuzi
:Mteja: Hapa.
Badala ya kusema Nani anahitaji wali na nyama ya mbuzi mhudumu ameokoa muda kwa kusema Nani wali mbuzi.


(ii) Rejesta hutumika kukuza lugha. Mfano; Baadhi ya rejesta ambazo hutumika mala kwa mala mtaani huwe za kusanifishwa na kuwa lugha rasmi hivyo husaidia kukuza lugha.

(iii) Rejesta husaidia kutunza siri Mfano: Rejesta za hospitalini kati ya mgonjwa na daktari; Hutumia rejesta ambazo hazitoi siri ya ugonjwa au madhaifu fulani aliyonayo mgonjwa.


(iv) Rejesta huburudisha na kuelimisha jamii. Mfano; Rejesta mbalimbali ambazo hutumiwa mitaani nyingi huwa zina burudisha jamii lakini zile zinazo tumika katika maeneo maalumu huelimisha jamii; kama vile rejesta za kazini, kanisani na msikitini.

**Kielelezo Na. 2.1**: Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2.

Watahiniwa 1,850 sawa na asilimia 8.9 walifanya swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kuandika kwa usahihi baadhi ya rejesta na matumizi yake na kushindwa kuandika rejesta nyingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kwa mifano ambapo alitoa maana ya rejesta na alifafanua matumizi manne ya rejesta kama vile: *kutumika kurahisisha mawasiliano, kutumika kuokoa muda, kupunguza ukali wa maneno na kuficha mazungumzo ya watumiaji* lakini maelezo yake hayakujitoshereza.

Aidha, watahiniwa 1,034 sawa na asilimia 5 walipata alama za chini kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kufasili rejesta kimakosa kwa kutoa maana ya misimu na wengine walielezea aina za rejesta na sifa za rejesta kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa fasili kuwa rejesta ni *matumizi ya lugha kulingana na mazingira uliyopo au eneo husika* na alishindwa kufafanua matumizi ya rejesta kwa kujibu *hotelini, hospitalini, kanisani na shuleni* badala ya kufafanua matumizi ya rejesta kama vile kutambulisha wazungumzaji, kuficha ujumbe na husaidia kukuza lugha. Kielelezo 2.2

kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama za chini.


2. (a) Rejesta ni matumizi ya lugha kulingana na mazingira uliyopo au eneo husika.


(b) Matumizi manne ya rejesta ni
i) Hotelini - chai mbili na Cd moja
ii) Hospitalini - Nesi huyu anatakiwa kuchomwa sindano.
iii) Kanisani - Bwana Yesu asifiwe, haleluya.
iv) Shuleni - Kalamu, daftari zimepotea.

**Kielelezo 2.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi kwa swali la 2.

### 2.2.3 Swali la 3: Matumizi ya Sarufi


Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa maana ya istilahi alizopewa kama zinavyotumika katika lugha ya Kiswahili. Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi*, mada ndogo ya *Matawi ya Sarufi* na lililenga kupima kumbukumbu. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Watahiniwa 20,767 sawa na asilimia 99.9 walijibu swali hili na miongoni mwao watahiniwa 20,398 sawa na asilimia 98.2 walifaulu kwa kiwango kizuri na kile cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3.5 hadi 10. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 3**: *Ufaulu wa Watahiniwa Kiasilimia*

Jumla ya watahiniwa 18,988 sawa na asilimia 91.4 walifanya swali hili na walifaulu vizuri kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 10. Kati yao watahiniwa 13,575 sawa na asilimia 65.4 walipata alama za juu zaidi kuanzia 8 hadi 10 kwa kuwa walitambua maana za istilahi walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa maana ya kipengele (a) sarufi kuwa *ni tanzu ya lugha inayohusika na maana, matamshi, miundo na maumbo ya lugha husika*, kipengele (b) mzizi wa neno *ni kipande kidogo cha neno ambacho hakiwezi kuvunjwavunjwa na kupata maana kisarufi* pia aliweza kutoa maana sahihi katika kipengele (c) na kipengele (d) hivyo, kupata alama za juu. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.


3 (a) Sarufi ni tanzu ya lugha inayohusika na maana, matamshi, miundo na maumbo ya lugha husika.
(b) Mzizi wa wa neno ni kipande kidogo cha neno ambacho hakiwezi kuvunjwavunjwa na kupata maana kisarufi
(c) Sarufi maumbo ni aina ya sarufi ambayo inahusika na uumbaji wa maneno kwa kuangalia viambishi.
(d) Sarufi matamshi ni aina ya sarufi ambayo inajihusisha na utamkaji wa maneno kwa kutumia irabu na konsonanti.


**Kielelezo Na. 3.1**: Sampuli ya majibu sahihui ya mtahiniwa aliyepata alama nzuri.

Watahiniwa 1,410 sawa na asilimia 6.8 walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 baada ya kutoa majibu sahihi kwa baadhi ya vipengele na majibu

yasiyo sahihi kwa vipengele vingine. Mfano, mtahiniwa mmoja alitoa maana sahihi ya sarufi na mzizi wa neno lakini alishindwa kabisa kutoa maana ya sarufi maumbo na sarufi matamshi.

Hata hivyo, watahiniwa 369 sawa na asilimia 1.8 walijibu swali hili na kupata alama za chini kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kushindwa kutoa maana sahihi za istilahi walizopewa. Watahiniwa hao walitoa maana za istilahi bila kuhusisha na mada ya sarufi. Mathalani, mtahiniwa mmoja alishindwa kutoa majibu sahihi kwa kuandika katika kipengele (a) sarufi *ni maumbo ambayo yanaundwa kwa kutumia maneno ili yaweze kuleta maana ili yatumiwe katika mawasiliano* badala ya Sarufi ni kanuni na taratibu za lugha zinazotumika ili kupata ufasaha na usanifu katika lugha.

kipengele (b) *mzizi wa neno ni maneno yanayotenganisha kiambishi awali na tamati ili kuweza kuleta maana* badala ya *umbo la msingi la neno ambalo haliwezi kuchanganuliwa tena katika maumbo mengine pasi na kupoteza maana ya neno*, kipengele (c) *sarufi maumbo ni aina ya sarufi ambayo imeundwa kulingana na muonekano wa maneno hayo au herufi hizo* badala ya sarufi *maumbo ni tawi la sarufi linalojishughulisha na uchambuzi wa mfumo wa maneno katika lugha* vivyo hivyo, katika kipengele (d) hakuweza kujibu kwa usahihi. Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa maana ya istilahi alizopewa.


3 (a) Sarufi, Ni maumbo ambayo yaundwa
kwa kutumia maneno ili yaweze kule
ta maana ili yatumike katika mawa
- siliano. Mfano sarufi a, .

(b) Mzizi wa neno. Ni maneno ambaye
yanatenganisha kiambishi awali na
kiambishi tamati ili kuweze kuleta
maana kwa mfano
- Alicheza
| chez ni mzizi wa neno
- Aliimba
| imb ni mzizi wa neno
- Anasoma
| som ni mzizi wa neno

(c) (i) Sarufi maumbo, Ni aina ya sarufi
ambayo inatengeneza maana ya neno
halisi ili iweze kuleta maana kwa
mfano umbo la herufi a, e, i, o ili
kuweza kuunda maneno zama.
-oa
- ua


(ii) Sarufi matamshi, Ni aina ya sarufi
ambayo imeundwa kulingana na muoneka
no wa maneno hayo au herufi hizo
ili ziweke kutamkika kwa kuangalia

**Kielelezo Na. 3.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 3.

### 2.2.4: Swali la 4: Matumizi ya Sarufi


Swali hili lilikuwa na vipengele (a) na (b): Kipengele (a) mtahiniwa alitakiwa kutumia –o-rejeshi kuandika upya sentensi alizopewa na kipengele (b): kuweka nomino alizopewa katika ngeli husika kwa kigezo cha kisintaksia. Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Sarufi*, mada ndogo ya *Matumizi ya O-rejeshi* na *Ngeli za Nomino*. Swali lililenga kupima uundaji na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali lilikuwa la lazima hivyo watahiniwa 20,772 sawa na asilimia 99.9 walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri kwa kuwa asilimia 93.3 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na kile cha wastani. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 4**: *Ufaulu wa Watahiniwa Kiasilimia*

Data zinaonesha kuwa, watahiniwa 3,863 sawa na asilimia 56.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata alama za juu kuanzia 6 hadi 10. Watahiniwa 9,241 sawa na asilimia 44.5 walipata alama za juu zaidi kuanzia 8 hadi 10 kwa kuwa waliweza kutumia –O-rejeshi katika kuandika upya sentensi na waliweza kuweka nomino katika ngeli husika kwa kigezo cha kisintaksia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kuandika sentensi kwa kutumia –O-rejeshi –cho-, -lo-, na -o- na pia aliweza kuweka nomino alizopewa katika ngeli za PA-MU-KU, LI-YA, KI-VI, I-ZI na U-YA. Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili vizuri.


4 a) ii) Shairi aliloghani ni zuri.
iii) Kiti alichonunua ni kibovu.
iv) Nazi aliyoivunja ni mbovu.
v) Ugonjwa alioupata haujulikani.
b) Weka nomino zifuatazo katika ngeli husika kwa kigezo cha kisintaksia.
i) Mahali — PA – MU – KU.
- Mahali - pale panafaa
- Mahali mule munafaa
- Kwahali kule kunafaa.
ii) Shairi — LI – YA.
- Shairi lile linaimbika
- Mashairi haya yanaimbika.
iii) Kiti - KI – VI.
- Kiti kimekatika
- Viti - vimekatika.
iv) Nazi - I – ZI
- Nazi imeanguka
Nazi zimeanguka.
v) Ugonjwa — U – YA
Ugonjwa umeenea.
Magonjwa yameenea.


**Kielelezo Na 4.1**: Sampuli fasaha ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Watahiniwa 7,618 sawa na asilimia 36.7 ya waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 3.5 hadi 5.5 kutokana na kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa kujibu baadhi ya vipengele. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishidwa kutumia –O- rejeshi kuandika upya sentensi kwa nomino alizopewa, lakini aliweza kuweka nomino katika ngeli husika kwa kigezo cha kisintaksia kama vile: (i) *mahali ali**po**ingia pana chatu* badala ya *mahali ali**mo**ingia mna chatu (ii) ali**vyo**ghani shairi zuri sana* badala ya *shairi ali**lo**ghani ni zuri sana (iii) ali**po**nunua kiti kibovu badala ya kiti ali**cho**nunua ni kibovu* lakini alijibu kwa usahihi katika kipengele (b) kwa kuweka nomino alizopewa katika ngeli zake mfano (i) mahali ngeli ya PA - MU – KU, (ii) shairi ngeli LI – YA, (iii) kiti ngeli ya KI – VI (iv) nazi ngeli ya I - ZI na (v) ugonjwa ngeli ya U - YA hivyo, ufaulu wa kiwango cha wastani.

Hali kadhalika, watahiniwa 1,391 sawa na asilimia 6.7 ya waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu hafifu kwa kupata alama kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kushindwa kutumia –O-rejeshi katika kuandika upya sentensi na kushindwa kuweka nomino katika ngeli husika kwa kigezo cha kisintaksia. Pia

watahiniwa wengine, waliunda sentensi ambazo hazikuwa na O rejeshi ndani yake kutokana na kuwa na mawanda madogo ya maarifa juu ya kutumia –O-rejeshi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alishindwa kabisa kutumia –O-rejeshi kuandika upya sentensi *(i) aliyeingia mahali mna chatu* badala ya *mahali alimoingia mna chatu, (ii) aliyeghani shairi zuri sana* badala ya *shairi aliloghani ni zuri sana,* (iii) *aliyenunua kiti kibovu* badala ya kiti achonunua ni kibovu, (iv) *aliyevunjiwa nazi mbovu* badala ya nazi aliyoivunja ni mbovu na (v) *aliyepata ugonjwa ambao haujulikani* badala ya ugonjwa uliompata haujulikani.

Vile vile, katika kipengele (b) alishindwa kuandika ngeli za nomino katika nomino alizopewa kwa kigezo cha kisintaksia kwa kuandika sentensi mpya kwa kutumia nomino badala ya kuonesha ngeli zinazopaswa kubeba nomino hizo. Kielelezo Na 4.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini.




**Kielelezo Na 4.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 4.


### 2.3.1 SEHEMU B.

Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali matatu kati ya maswali manne yaliyopo katika sehemu hii. Kila swali lilikuwa na alama ishirini (20).

### 2.3.2 Swali la 5: Utungaji


Mada hii ya *Utungaji* ilikuwa na swali moja ambalo lilipima *uundaji*. Swali lilimtaka mtahiniwa kuandika kadi ya kuomba mchango wa harusi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Uchambuzi wa data za ufaulu wa watahiniwa unaonesha kuwa, swali hili lilifanywa na watahiniwa 11,570, kati yao watahiniwa 11,274 walilijibu vizuri na walifaulu vizuri na wastani. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 5**: *Ufaulu wa Watahiniwa Kiasilimia*

Watahiniwa 9,195 sawa na asilimia 79.5 walikuwa na ufaulu mzuri kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 20. Miongoni mwao, watahiniwa 810 walipata alama za juu kuanzia 18 hadi 20 kutokana na kuweza kuandika kadi ya mchango wa harusi kwa kufuata vigezo kama vile: *kichwa cha kadi, jina la familia inayoomba mchango, mahali ilipo, jina la mwandikiwa, lengo la taarifa, tarehe ya mwisho ya kuwasilisha mchango, njia ya mawasiliano, matumizi ya lugha fasaha, alama za uandishi na ubunifu*. Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.


5:

KADI YA KUOMBA MCHANGO WA HARUSI.

Familia ya Mzee Tumaini wa Musoma mjini inayofurahia kukuomba mchango wa harusi.

~~Mwl~~/~~Bw~~/~~Bibi~~/Askofu/~~Adg~~

MICHAEL MJONKANZIRA:

Mchango huo ni wa harusi ya binti yao mpendwa JIKUDHANI TUMAINI anayetarajia kufunga ndoa Tarehe 15/6/2020 nyumbani kwao Musoma. Ukiwa kama ndugu na rafiki wa karibu tunaomba mchango wako ili kufanikisha harusi hiyo. Mchango huo ni shilingi 50000/= hamsini elfu na mwisho wa mchango ni Tarehe 10/05/2020 mpe mchango aliyekupa kadi hii kwa mawasiliano zaidi piga

0756371435 Mwenyekiti


0674441700 Mhazini

kutoa ni moyo na sio utajiri.

**Kielelezo Na. 5.1**: Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Watahiniwa 2,086 sawa na asilimia 18 walipata alama za wastani kuanzia 6.5 hadi 11.5 kwa kuwa waliweza kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa vipengele vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kadi ya kuomba mchango wa harusi na kushindwa kuonesha jina la aliyekuwa anaombwa mchango, hakuonesha tarehe ya mwisho wa kupokea mchango ila aliandika kwa usahihi tarehe ya harusi hiyo na alionesha mahali itakapo fanyika hivyo, alipata alama za wastani.

Vilevile watahiniwa 289 sawa na asilimia 2.5 ya waliofanya swali hili walipata alama za chini kuanzia alama 0 hadi 6.5. Watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uandishi wa kadi za kuomba mchango wa harusi na hawakufuata kanuni za uandishi na wengine waliandika barua za kikazi badala ya kadi ya mwaliko. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja badala ya kuandika kadi ya kuomba mchango wa harusi aliandika barua ya kirafiki/kindugu. Kielelezo Na. 5.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili na kupata alama za chini.


5.

S. L. P. 20,
TUNDUMA.
10/6/2020.

Mpendwa, Sikudhani Jumaini.

Natumaini u mzima wa afya. Kwa upande wangu ni buheri kabisa. Habari za mihangaiko na hongera kwa hatua uliyoifikia rafiki yangu.

Dhumuni la kuandika barua hii ni kukuomba kuwa usinisahau katika harusi yako itakayofanyika tarehe 15/6/2020. Hivyo naomba kadi ili niweze kukuchangia katika harusi yako na kuhudhuria katika sherehe ya ndoa yako.


Ni mimi,
Chausiku Juma.

**Kielelezo Na. 5.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 5.

### 2.3.3 Swali la 6: Maendeleo ya Kiswahili

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* na lililenga kupima *kuchambua*. Mtahiniwa alitakiwa kubainisha mambo sita yanayosaidia kukua na kuendelea kwa Kiswahili duniani. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Watahiniwa 19,808 walijibu swali hili ambalo lilikuwa la kuchagua. Swali hili ni miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 99.5 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri na wa wastani. Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 6** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Data inaonesha kwamba, watahiniwa 19,808 sawa na asilimia 87.3 walifaulu vizuri kwa kupata alama kuanzia 12 hadi 20 baada ya kuweza kubainisha mambo sita yanayosaidia kukuza na kuendeleza Kiswahili duniani kama vile: *(i) urahisi wa lugha yenyewe (ii) vyombo vya habari (iii) utumizi katika nyanja ya elimu (iv) kutumika katika mikutano ya kimataifa (v) kutumika katika biashara, dini na sanaa (vi) kukua kwa matumizi ya mitandao*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha mambo yanayosaidia kukuza na kuendeleza Kiswahili duniani kama vile: *namna elimu ilivyotumika*, *vyombo vya habari duniani mfano BBC, VOA, na DW*. Vilevile, alielezea *sanaa na burudani* na *kuundwa kwa asasi mbalimbali za ndani na nje ya nchi kama vile: CHAKIKE, CHAKA na TATAKI*. Kielelezo Na. 6.1 ni sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili vizuri.

6. Kiswahili ni lugha yenye asili ya kiafrika iliyotokana na lugha za kibantu na huzungumzwa sana Afrika mashariki yaani katika nchi za Afrika mashariki kama vile Tanzania, Kenya, Uganda, Somalia, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na sehemu nyingine kwa uchache kama vile Zambia, Mozambiki au msumbiji, Afrika ya kusini na Sudani. Kukua na kuendelea kwa kiswahili duniani kumechangizwa na kupata huru kwa nchi ya Tanganyika. Yafuatayo ni mambo yanayosaidia kukua na kuendelea kwa kiswahili duniani.

Elimu; kiswahili kimekuwa kikifundishwa katika ngazi ya juu ya elimu hivi karibuni kwa ngazi ya stashahada na shahada katika vyuo vikuu mbalimbali hapa duniani. Kwa mfano katika chuo kikuu marekani kiitwacho "University of california, chuo kikuu nchini china, OXFORD university cha nchini uingereza, chuo kikuu cha makerere nchini Uganda. Hivyo basi kwa kuendelea kuzalishwa wataalamu mbalimbali wa lugha ya kiswahili kutoka vyuo vikuu, kiswahili kinakua na kuenea duniani.

Vyombo vya habari; kumekuwa na matumizi ya lugha ya kiswahili katika vyombo mbalimbali duniani vikitoa habari kwa kutumia lugha ~~toy~~ ya kiswahili katika nchi mbalimbali duniani. Kwa mfano shirika la utangazaji la uingereza "British Broadcasting Conporation" BBC, DW swahili, Sauti ya America VOA, Redio sauti ya Japani. Hivyo basi matumizi ya lugha ya kiswahili katika vyombo hivyo kunapelekea kiswahili kukua duniani.

Sanaa na burudani; Pia sanaa na burudani ya kiswahili inamchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza kiswahili duniani. Mfano sanaa ya muziki, Bongo Flava hutumika katika majukwaa mbalimbali duniani na husikilizwa na watu mbalimbali duniani; Pia tamasha la SAUTI ZA BUSARA linalofanyika Zanzibar na kukutanisha watu kutoka mataifa mbalimbali duniani; Hivyo basi kwa kupitia sanaa na burudani kiswahili hukua na kuendelea duniani.

Shughuli za kitalii; kwa kupitia wageni wanaoingia nchini kutoka mataifa mbalimbali duniani kuja kufanya utalii nchini Tanzania katika mbuga za wanyama kama vile serengeti, ngorongoro na Masaimara, Pia katika mlima Kilimanjaro. Kwa kupitia utalii wageni hupenda kujifunza tamaduni za wenyeji wa Tanzania ikiwamo kutambua uwepo wa lugha ya kiswahili nchini Tanzania na wengine hupendelea kujifunza za lugha ya kiswahili. Hivyo basi kiswahili hukua na kuendelea duniani pale wageni wanaporudi katika nchi zao.

Kuundwa kwa asasi mbalimbali nje ya nchi ya Tanzania za kukuza na kueneza kiswahili; Asasi hizo zimekua zikifanya uchunguzi wa lugha ya kiswahili na kuhamasisha matumizi ya lugha ya kiswahili nje ya Tanzania. Mfano CHAMA CHA KISWAHILI KENYA (CHAKIKE), CHAMA CHA KISWAHILI AFRIKA (CHAKA). Asasi hizo zimekua zikichangia sana kukua na kuendelea kwa kiswahili duniani kote.

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya majibu ya majibu sahihi katika swali la 6.

Idadi ya watahiniwa 2,411 sawa na asilimia 12.2 walifanya swali hili na kupata alama za wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 kutokana na kubainisha mambo yanayosaidia kukua na kuendelea kwa Kiswahili duniani kwa usahihi lakini alishindwa kuelezea kwa mapana hoja zake. Mathalani, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *vikundi vya Sanaa, mikutano mikubwa, vyuo na shughuli za utalii* lakini alishindwa kueleza kwa mapana hoja hizi hivyo, alipata alama za wastani.

Mchanganuo zaidi wa data unaonesha kwamba, watahiniwa 98 sawa na asilimia 0.5 walipata alama za chini kuanzia 0 hadi 6.5 baada ya kushindwa kubainisha mambo yanayosaidia kukua na kuendelea kwa Kiswahili duniani. Wengi wao walitoa sababu za kuenea kwa Kiswahili Tanzania na wengine walielezea hoja za kukua kwa Kiswahili kulikosababishwa na wakoloni jambo ambalo ni kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea mambo yaliyosaidia kukua na kuendelea kwa Kiswahili Tanzania kabla ya uhuru kama vile: *ujenzi wa reli ya kati, harakati za kudai uhuru, biashara kabla ya uhuru* badala ya kueleleza mambo yaliyokuza na kuendeleza Kiswahili duniani. Hii inathibitisha kuwa mtahiniwa alikosa maarifa ya kutosha kuhusu maendeleo ya Kiswahili duniani. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyeonesha sababu za kukua kwa Kiswahili Tanzania badala ya kukua kwa Kiswahili duniani.


| | |
|---|---|
| 6. | kukua kwa kiswahili; Ni ile hali ya |
| | lugha ya kiswahili kuongeza misamiati mpya kati |
| | ka mawasiliano; misamiati inaweza kuongezeka kwa |
| | njia ya Utohoaji, mfano neno Safari, Urudufishaji na |
| | mengineyo mengi. Pia kiswahili kilikua na kuenea |
| | nchini Dunia kabla ya uhuru kwa nchi za Afrika |
| | Mfano katika Utawala wa Mgerumani na |
| | Utawala wa mwingereza. Hivyo basi kumbe |
| | hata kabla ya Uhuru kiswahili kilikua na |
| | kuendelea duniani pote kwa kuwa kilitumiaka |
| | katika shunghuli mbali mbali. yafuatayo ni - |
| | Mambo yaliyochangia kukua na kuendelea kwa - |
| | |

6 kiswahili duniani. mambo hayo ni kama -
Inpuatavyo.
Utawala; kabla ya Uhuru utawala wa
kikoloni ulichangia kukua na kuendelea kwa kiswa
hili duniani. Mfano katika Utawala wa Muinge
reza kiswahili kilitumika katika mawasiliano.
Pia ulitualazimu kwa wageni wasio jua kiswa
hili wajifunze kwanza ili waweze kufa
nya kazi katika Serikali ya kikoloni. Mfano
Muingereza alifanya hivyo nchini Tanganyi
ka, na Kenya. Pia kipindi cha mjerumani
kilitumika katika nyanja za Utawala; Hivyo
suala la Utawala wa kikoloni ulichangia
kukua kwa kiswahili duniani.
Dini; Wamishinari wakati waneene
za dini Afrika walijifunza kwanza wao lugha
ya kiswahili ili iweze kuwasaidia katika
kuhubiri dini yao ya kikristo. Hivyo walikuza
lugha ya kiswahili katika makazi yao na
Afrika kwa Ujumla. Mfano Waingereza
walitumia lugha ya kiswahili katika
kutelea maadili yao ya kidini mfano
nchi kama Tanganyika, kenya.
Ujenzi wa reli ya kati; kabla ya
Uhuru wa Afrika wajerumani walijenga reli
ya kati ili kurahisisha usafirishaji wa
Malighafi. Hivyo wafanyakazi walikuwa
wakijenga reli hiyo waliamuliwa wajifu
nze lugha ya kiswahili ili watumie
katika mawasiliano. hivyo ilisaidia kukua
za lugha ya kiswahili kwa wazao wa
lugha hiyo na kwa wageni ambao ni wakoloni

**Kielelezo Na. 6.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 6.

### 2.3.4 Swali la 7: Maendeleo ya Kiswahili

Uchambuzi unaonesha kuwa swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* katika mada ndogo ya *Usanifishaji wa Kiswahili*. Swali lilimtaka mtahiniwa atathmini upungufu uliojitokeza wakati wa kusanifisha Kiswahili kabla ya uhuru kwa kutoa hoja sita. Swali lililenga kupima tathmini na lilikuwa na jumla ya alama 20. Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. *7:*** *Ufaulu wa atahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 9,999 sawa na asilimia 98.3 ya watahiniwa 10,030 waliofanya swali hili, walikuwa na ufaulu mzuri na wa wastani kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu usanifishaji wa Kiswahili kabla ya uhuru.

Miongoni mwao, ya watahiniwa 8,175 sawa na asilimia 80.4 waliofanya swali hili walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 12 hadi 20. Kati yao, asilimia 3.6 walipata alama za juu zaidi kuanzia 18 hadi 20 kwa kuwa walikuwa na weledi wa kutathmini upungufu uliojitokeza wakati wa kusanifisha Kiswahili kabla ya uhuru kama vile: *Kiswahili kusanifishwa na wageni, kutokubalika kwa lahaja ya kiunguja, uhaba wa vitabu, uhaba wa fedha na machapisho yaliyotolewa yalikuwa na makosa mengi.* Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

07. Lugha ya Kiswahili ilisanifishwa na wageni wa Kiingereza wakati wa Utawala wa Mwingereza nchini Tanzania kabla ya Uhuru. Waingereza waliunda Kamati ambayo ilikuwa na jukumu kubwa la kusanifu Lugha ya Kiswahili. Aidha waliteua Lahaja ya Kiunguja ili itumike kama Lahaja ya Kisanifu Kiswahili yafuatayo ni mapungufu mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa kusanifisha Kiswahili kabla ya Uhuru.

Uhaba wa fedha; katika harakati za kusanifisha Kiswahili, Kamati ya Usanifishaji ilikumbana na tatizo la Upungufu wa fedha kwa ajili ya kuendeshea shughuli mbalimbali za Usanifishaji, ikiwa pamoja na kutoa machapisho mengi zaidi ili yaweze kuwafikia watu wengi.

Uhaba wa Vitabu; Wakati wa Usanifishaji wa Lugha ya Kiswahili, Kamati haikuweza kuchapisha vitabu vingi vya Kiswahili sanifu. hivyo kupelekea Upungufu wa Vitabu vya Kiswahili sanifu. Vitabu hivyo vichache havikuweza kukidhi idadi ya watu na hivyo kuishia kusomwa na watu wachache.

Kiswahili kusanifiwa na wageni; Kamati iliyoundwa kwa lengo la kusanifisha Lugha ya Kiswahili ilikuwa na mapungufu yake. Kwani Kamati hiyo haikuwahusisha wenyeji na badala yake iliundwa na wageni tu ambao siyo wazawa wa Tanganyika na

07. Hivyo Kupelekea upungufu katika zoezi la Kusanifisha Kiswahili.

Watu Kutosoma machapisho yaliyotolewa na Kamati ya Usanifishaji; Wakati wa Usanifishaji, watu hawakuwa na desturi ya Kujisomea machapisho (vitabu) yaliyotolewa na Kamati. hivyo machapisho hayo ya Kiswahili sanifu yaliishia tu Kusomwa na watu wachache na hivyo Kupelekea changamoto katika zoezi La Usanifishaji.

Kutokubalika kwa Lahaja ya Usanifishaji; pia katika zoezi la Usanifishaji wa Kiswahili, Lahajia ya Kiunguja, ambayo ilitenliwa Kama Lahaja ya Kusanifu kiswahili haikukubalika na watu ili itumike Kama lahaja ya Kusanifu Kiswahili Kwani watu walikosia Kudumaa Kwa Lahaji nyinginezo, na hivyo Kupelekea upungufu.

Tatizo La msamiati; Wakati wa Usanifishaji Kulikuwa na tatizo la Kimsamiati, Mfano inje - nje, Inge - nge. Kwa Kuwa Lugha ya Kiswahili ilisanifiwa na wageni tu, hivyo ikapelekea Kutokea Kwa upungufu huo wa Kimsamiati.

Hivyobasi, Mbali na Kujitokeza Kwa upungufu huo, bado Kamati ya Usanifishaji ilipambana na Kufanikisha zoezi zima la Usanifishaji, Lugha ya Kiswahili ilipata Kusanifishwa na ndiyo lugha hii tunayoitumia Leo hii Kama Lugha ya taifa nchini Tanzania

**Kielelezo 7.1**: Sampuli ya majibu fasaha ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Idadi ya watahiniwa waliopata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 ni 1,824 sawa na asilimia 17.9. Watahiniwa hawa walitathimini hoja chache ambazo hazikutosheleza kuonesha upungufu uliojitokeza wakati wa kusanifisha Kiswahili kabla ya uhuru. Mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutoa hoja kama vile: *ufafanuzi wa baadhi ya semi ulikosewa, usanifishaji haukushirikisha wenyeji, kutokubalika kwa lahaja ya kiunguja* lakini alishindwa kutoa maelezo yaliyojitosheleza.


Takwimu zaidi za uchanganuzi zinaonesha kuwa, watahiniwa asilimia 1.7 waliofanya swali hili walikuwa na kiwango cha chini cha ufaulu wa kupata alama kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kuwa na uelewa mdogo na kushindwa kuelewa madai ya swali katika mada usanifishaji wa lugha ya kiswahili. Watahiniwa hao walitoa hoja ambazo zilikuwa hazijibu swali; mfano, *uhaba wa pesa* na wengine walielezea usanifishaji baada ya uhuru, halikadhalika wengine walielezea faida za usanifishaji kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja hakuweza kutathmini upungufu ulijitokeza wakati wa kusanifisha Kiswahili kabla ya uhuru kwa kushindwa kutoa dhana ya Kiswahili na pia aliandika *kutokubalika kwa lahaja ya usanifishaji iliyoteuliwa na uhaba wa machapisho* na *upungufu wa kutohusishwa kwa lahaja zingine za kibantu, kutumika kwa muda mwingi wa usanifishaji* jambo ambalo halikuwa kweli badala yake alitakiwa kuandika *kutokubaliwa kwa lahaja ya usanifishaji iliyoteuliwa*, *machapisho yaliyotolewa na kamati ya lugha yalikuwa na makosa mengi* na *uhaba wa wataalam*. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kutoa tathmini kuhusu upungufu uliojitokeza wakati wa kusanifisha Kiswahili kabla ya uhuru.

9. Kabla ya uhuru wa Tanzania lugha ya Kiswahili iliweza kusanifiwa na Waingereza waliokuja kwa lengo la kutawala Tanzania. Waingereza waliunda Kamati ya Usanifishaji iliyoitwa Enter-Territorial Language Commitee ambayo ilitakiwa kufanya shughuli nzima ya usanifishaji; Lakini wakati shughuli ya usanifishaji inaendelea kuna baadhi ya mapungufu yalijitokeza. Miongoni mwa mapungufu hayo ni kama yafuatayo:-

Dhana ya Kiswahili ilitolewa kwa lugha ya Kiingereza; Kamati iliyokuwa imeundwa na Waingereza kwa lengo la kusanifisha lugha ya Kiswahili ilitumia lugha ya Kiingereza kutoa maana ya Kiswahili. na wakati ilitumia watumie lugha hiyohiyo inayosanifiwa. Hivyo ikapelekea kazi ya usanifishaji kuonekana ina map

Kutowahusisha wenyeji wa lugha ya Kiswahili katika shughuli nzima ya usanifishaji; Kamati iliyoundwa kwa ajili ya kusanifisha Kiswahili haikuweza kuwahusisha wenyeji wa lugha ya Kiswahili katika shughuli nzima ya usanifishaji.

Kutohusishwa kwa lahaja zingine za Kibantu; Kamati iliyokuwa imeundwa na Waingereza wakati wa usanifishaji hawakuweza kuzihusisha lahaja zingine katika kusanifisha lugha ya Kiswahili; walitumia lahaja moja tu iliyokuwa imekuwisha teuliwa ambayo ilikuwa ni lahaja ya Kiunguja tu kutokana na kufanyika ~~kwa~~ au kutumika kwa Kiunguja tu imepelekea kutokea kwa n



7 Kutumia kwa baadhi ya maneyo ya
Kiingereza katika lugha ya Kiswahili; katika
shughuli ya kukisanifisha Kiswahili wanakamati
waliweza kutumia baadhi ya misamiati ya
Kiingereza katika lugha ya Kiswahili wakati
swali ilikusudiwa kutumia lahaja ya Kiunguja
tu. Mfano neno shati, kompyuta na prozram.
Kiswahili kutotumika maeneo yote yaliyo-
kusudiwa, baada ya usanifishaji lugha ya Kiswahili
haikuweza kutumiwa na maeneo yote yale yaliyo-
kusudiwa. Mfano Rwandwa na Kenya. Hivyo kutokana na
kutotimia kwa malengo yaliyokusudiwa imepelekea
shughuli ya usanifishaji kuwa na mapungufu.
Kutumika kwa muda mwingi
zaidi wakati wa usanifishaji; kutokana
na kamati ya usanifishaji kutumia muda
mwingi zaidi katika kusanifisha lugha
ya Kiswahili imepelekea shughuli hii kuw
na mapungufu.
Hivyo; sio kusamba kabla ya uhuru
katika shughuli ya usanifishaji ilikuwa na
mapungufu tu lakini pia shughuli hii ili-
weza kufanikiwa kwa baadhi ya mambo.
Miongoni mwa mambo hayo ni kama kurahi-
sisha mawasiliano, kusawazisha matamshi ya
lugha ya Kiswahili.

**Kielelezo Na. 7.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 7.

### 2.3.5 Swali la 8: Tafsiri na Ukalimani

Swali lilimtaka mtahiniwa afafanue changamoto tano zinazojitokeza katika kufasiri matini za kifasihi. Swali lilihusu mada ya *Kutafsiri na kukalimani* na mada ndogo ya *tafsiri*. Swali lililenga kupima kuchambua na lilikuwa na jumla ya alama 20.

Watahiniwa wote (20,784) walijibu swali hili. Asilimia 69.7 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na kile cha wastani. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya ufaulu vya watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na.8** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Jumla ya watahiniwa 3,808 sawa na asilimia 18.3 walijibu swali hili na kupata alama nzuri kuanzia 12 hadi 19.5 kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kufasiri matini za kifasihi. Watahiniwa walionesha kuwa katika kufasiri matini za kifasihi, kunaweza kujitokeza changamoto mbalimbali kama vile: *matini kuandikwa kwa lugha ya kisanii hali inayosababisha changamoto kubwa katika kufasiri, matini kushindiliwa dhana mbalimbali za kiutamaduni pia kutozingatia kizio cha maana* ni changamoto zinazoweza kujitokeza wakati wa kutafsiri matini za kifasihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu vizuri swali hili kwa kufafanua changamoto tano zinazojitokeza katika kutafsiri matini za kifasihi kama vile: *tofauti za kiitikadi, tofauti za kifasihi, tofauti za kimuundo, tofauti za kiutamaduni na tofauti za kimtindo*. Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama nzuri kutokana na kujibu vizuri swali hili.

8 Kutafsiri ni kitendo cha kuhawilisha mawazo, maarifa au ujumbe uliopo kwenye matini chanzi kwenda kwenye matini lengwa. Mtu anayetafsiri matini huitwa Mfasiri. Wakati wa kutafsiri mfasiri hukutana na changamoto mbalimbali ambazo ni kama zifuatazo.

Tofauti za kiitikadi, wakati wa kutafsiri matini za kifasihi kunaweza kujitokeza tofauti za kiitikadi kwa mfasiri, Hivyo kufanya matini kueleweka tofauti na malengo. Mfano katika kitabu cha "Merchant of Venis" Ambacho alikitafsiri Mwl. J.K Nyerere alikitafsiri kama "Mabepari wa Venis" hii ilitokana na tofauti za kiitikadi ambapo Nyerere aliamini kuamba "Merchant" ni bepari badala ya Mfanyabiashara

Tofauti za kiutamaduni / mazingira, Tofauti hii inaweza kusababisha matini kueleweka tofauti na lengo la matini chanzi. Hii hutokana na mfasiri kuwa na tamaduni tofauti na matini chanzi jambo ambalo linaweza kusababisha matini kueleweka tofauti.

Tofauti za kimuundo, Hii huleta changamoto wakati wa kutafsiri matini chanzi. Matini chanzi kama inakuwa na muundo ambao ~~matini lengwa~~ hutofautiana na muundo wa matini lengwa hali hii husababisha matini lengwa kutoeleweka vizuri.

Tofauti za kifasihi, Matumizi ya lugha za kifasihi ktk matini chanzi husababisha mfasiri ~~kuto~~ kushindwa kutafsiri kazi yake kwa ufanisi mfano, Matumizi ya nahau, Methali na tamathali za semi ktk matini chanzi huweza kusababisha mfasiri kutofaulu vizuri ktk kazi yake

| | |
|---|---|
| 8 | Tofauti za kimtindo, Mtindo wa lugha ambao ~~mt~~ matini chanzi umetumia huweza kumpa changamoto mfasiri na ashindwe namna ya ~~[illegible]~~ kubadilisha na kuweka ktk matini lengwa. |
| | Hivyo basi Mfasiri kabla hajaanza kazi yake ya kufasiri anatakiwa ajue kiundani utamaduni wa mwandishi wa matini chanzi ili iwe rahisi kwake kutafsiri kazi yake. |

**Kielelezo 8.1**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Vile vile, watahiniwa 10,678 sawa na asilimia 51.4 waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia alama 7 hadi 11.5 kutokana na kufafanua baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika kufasiri matini za kifasihi na kushindwa kufafanua changamoto nyingine. Mathalani, mtahiniwa mmoja alifafanua hoja kama vile: tofauti za *kiitikadi, kiutamaduni, kimaana na misemo, nahau na methali* lakini alitoa hoja isiyosahihi ya *matumizi ya nomino za pekee* tofauti kabisa na matakwa ya swali.

Watahiniwa 6,298 sawa na asilimia 30.3 walishindwa kujibu vizuri swali hili na kupata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa maarifa ya mada ya Tafsiri na Ukalimani na kushindwa kuelewa madai ya swali. Watahiniwa hao walielezea dhima za tafsiri na wengine walielezea mchakato wa zoezi la tafsiri kinyume kabisa na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua changamoto kama vile: *tafsiri tenge* akiwa na maana *kutokuwa na uhusiano kati ya matini chanzi na lengwa*, *tafsiri finyu* akiwa na maana ya *kuachwa kwa vitu vingi bila kufasiriwa* tafsiri pana akimaanisha ni *kuongeza maneno kwenye matini lengwa*. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua changamoto za kufasiri matini za kifasihi.


8. Kufasiri; ni kitondo cha kuhawilisha maneno yaliyopo katika maandishi kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine mfano kutoka kiingereza kwenda kiswahili. na katika kufasiri matini kuna mbinu mbalimbali ambazo huweza kutumika. kama Tafsiri ya neno kwa neno, ya kimawasiliano ya kisemantiki na Tafsiri sisisi mfano wash your hand. osha yako mikono. Zifuatazo ni changamoto zinazojitokeza katika kufasiri matini za kifasihi.

Tafsiri pana; hii ni changamoto ambayo inajitokeza katika kufasiri matini ya kifasihi. ni pale ambapo mfasiri anaongeza maneno kwenye matini lengwa ambayo hayakuwepo hata kwenye matini chanzi hivyo huweza kuonekana kama changamoto katika kufasiri matini ya kifasihi.

Tafsiri tenge; hii pia ni changamoto kwasababu hapa tunaona kuwa mfasiri anatafsiri matini ambapo mwisho wake tunakuwa hatuna uwiano wa matini lengwa na matini chanzi ni kwasababu anafasiri vitu ambavyo havipo katika matini chanzi hivyo kuonekana kuwa ni changamoto inayojitokeza katika kufasiri matini ya kifasihi.

Tafsiri finyu; pia hii nayo ni changamoto iliyojitokeza katika kufasiri matini za kifasihi. kwasababu hapa ~~mfasi~~ mfasiri huweza kuacha vitu vingi bila ya kuvifasiri katika matini lengwa hivyo ~~maneno~~ mengi katika matini chanzi huweza kuachwa bila kutafsiriwa hivyo kuwa ni changamoto iliyojitokeza katika kufasiri matini za kifasihi

Tofauti za kiisimu; ni changamoto


8. iliyojitokeza katika kufasiri matini za kifasihi
kwasababu mfasiri anashindwa kupata maana ya
moja kwa moja ya lugha husika mfano mercha-
nt of venice- mabepari wa venisi no smoking-
usivute sigara Tofauti-za
Tofauti za kiitikadi na kihisia; ni
changamoto mojawapo iliyojitokeza katika
kufasiri matini za kifasihi. hivyo mfasiri
huweza kufasiri matini husika kwa kuangalia
imani na hisia aliyonayo kuhusu maana ya
neno fulani mfano merchant of venice - mabe-
pari wa venisi.
Kwahiyo, kutokana na changamoto
hizo huweza kupelekea matini za kifasihi kuwa
na makosa mengi sana. ambapo muda mwingi
ne zinatumiwa hazina mvuto wowote.

**Kielelezo Na. 8.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 8.

## 3.0 SEHEMU YA II: MTIHANI WA KISWAHILI KARATASI YA PILI.

## 3.1 TATHMINI KWA KILA SWALI


## 3.2 SEHEMU A

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne ambayo mtahiniwa alitakiwa kuyajibu yote. Sehemu hii ina jumla ya alama arobaini na kila swali lilikuwa na alama 10.

### 3.2.1 Swali la 1: Fasihi Kwa Ujumla

Mtahiniwa alitakiwa kujibu hoja kuwa uhuru wa mwandishi ni zao bora la kazi za fasihi na kuonesha vipingamizi vitano (5) vinavyoingilia uhuru wa mwandishi na kusababisha kazi zake kupwaya. Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla*, mada ndogo ya *Uhuru wa Mtunzi wa kazi za Kifasihi*. Swali lililenga kupima kuelewa na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Uchanganuzi wa data unaonesha kuwa, swali hili lilijibiwa na watahiniwa 20,676 sawa na asilimia 99.5 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani. Ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri ambapo asilimia 63.8 walikuwa na ufaulu mzuri na wastani. Chati Na. 9 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa Kiasilimia*

Watahiniwa 6,349 sawa na asilimia 30.7 ya waliofanya swali hili walifanya vizuri na kupata alama za juu kuanzia 7 hadi 10. Hii inathibitisha kuwa, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya

*Uhuru wa Mwandishi* na kuelewa vema matakwa ya swali. Watahiniwa hao waliweza kuonesha vipingamizi vitano (5) vya uhuru wa mwandishi vinavyoweza kusababisha kazi zake kupwaya. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja sahihi kama vile: *udhamini, uwepo wa tabaka tawala itikadi, kuwepo kwa utawala wa dini na tamaduni mbalimbali za jamii.* Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyekidhi matakwa ya swali na kupata alama za juu.

1 (i) Udhamini.
Kudhaminiwa kwa mwandishi husababisha mwandishi kuandika yale tu ambayo mfadhili wake anayahitaji, hivyo mwandishi hukosa uhuru wa kujieleza vizuri.

(ii) Uwepo wa tabaka tawala.
Pia mwandishi hukosa uhuru kunapokuwepo na tabaka tawala, mwandishi huofia kuichokoza tabaka tawala na hivyo kuandika vitu vichache.

(iii) Itikadi.
Mitazamo pia ya watumbalimbali huingilia uhuru wa mwandishi, mwandishi anapoandika maelezo kuhusu jambo fulani huangalia itikadi za watu mbalimbali katika jamii juu ya jambo hilo.

(iv) Kuwepo kwa utawala wa dini.
Dini pia huingilia uhuru wa mwandishi, mfano riwaya ya "Roza Mistika" ilipingwa sana na waumini wa dini ya kikatoliki, wakieleza kuwa inakiuka maadili ya dini hiyo.

(v) Tamaduni mbalimbali za jamii.
Pia mwandishi wa kazi yoyote huangalia kunza tamaduni za jamii anayoiandikia kazi hiyo, baadhi ya jamii haziruhusu baadhi ya mambo kuelezewa kwa uwazi, hivyo humfanya mwandishi kukosa uhuru.

Kielelezo Na. 9.1 Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Aidha, watahiniwa 6,850 sawa na asilimia 33.1 walijibu swali hili na kupata alama za wastani kuanzia 4 hadi 6. Watahiniwa hao walieleza kwa usahihi baadhi ya vipingamizi na kushindwa kueleza vipingamizi vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alionesha vipingamizi kama vile; *Udhamini, utamaduni* na *udhibiti wa vitabu* kwa usahihi lakini vipingamizi kama *vyombo vya dola* na *vyombo vya habari* maelezo yake hayakujitosheleza hivyo kupata alama za wastani.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa hao unaonesha watahiniwa 7,477 ambao ni asilimia 36.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3. Watahiniwa hao walipata alama hafifu kutokana na kukosa maarifa na uelewa wa mada ndogo ya *Uhuru wa mtunzi wa kazi za kifasihi*. Baadhi ya watahiniwa walitoa dhima ya uhuru wa mwandishi na wengine walielezea athari za uhuru wa mwandishi kinyume kabisa na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea vipengele vya fani kama vile: *mtindo, muundo, mandhari, wahusika na matumizi ya lugha* badala ya kuonesha vipingamizi vinavyoingilia uhuru wa mwandishi. Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.

1. (i) Mtindo
— Ni namna ambavyo msanii amepangilia kufikisha ujumbe katika kazi ya fasihi kwa jamii.
Hivyo kama Mwandishi anatatumia Mtindo usio Mzuri kazi yake husindwa kuelewa na kupwaya.

(ii) Muundo.
— Ni Mpangilio wa Visa na Matukio katika Habari. Kama Mwandishi ataweza kuwa na Mpangilio Mbaya wa Visa na Matukio kazi yake hupwaya sana hivyo kushindwa kueleweka.

(iii) Madhari
— Ni Mahali ambapo kazi ya Fasihi hufanyika. Yaweza kuwa madhari halisi au madhari yasiyo halisi

(iv) Wahusika
— Ni jumla ya vitu vyote vinavyoshirikishwa katika kazi ya Fasihi. Yaweza kuwa miti, wanyama, binadamu na vingine.


(v) Matumizi ya lugha
— Ni namna ambavyo Mwandishi ametumia Misemo, Nahau, methali na Tamathali za semi katika kazi ya Fasihi.

**Kielelezo Na.9.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 1.

### 3.2.2 Swali la 2: Maendeleo ya Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Fasihi Simulizi* na lililenga kupima Kumbukumbu. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua kwa ufupi usemi usemao ‘‘Hadithi na sanaa za maonesho ni tanzu za fasihi simulizi zenye kufanana na kutofautiana’’ na kutoa hoja tatu za kufanana na hoja mbili za kutofautiana kwa tanzu hizo. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Mchanganuo wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa 14,054 sawa na asilimia 68.2 ya watahiniwa ndio waliojibu swali hili walikuwa na ufaulu mzuri na wastani. Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 10**: *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Mathalani, watahiniwa 6,743 sawa na asilimia 32.7 ya waliojibu swali hili walipata alama nzuri kuanzia 6 hadi 10 kutokana na kuwa na uelewa wa mada ya tanzu za fasihi simulizi. Miongoni mwao, watahiniwa 1961 walijibu vizuri swali hili na walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kufafanua usemi kwa hoja za kufanana na kutofautina kama vile; *zote mbili huwa na fanani na hadhira, zote mbili hutumia lugha* na *zote* lazima *ziwe na sehemu ya utendaji*, vile vile, alifafanua kwa usahihi hoja mbili za kutofautiana kwa tanzu hizo ambazo ni: *hadithi huweza kupokea mabadiliko ya papo kwa papo wakati sanaa za maonyesho haziwezi kupokea mabadiliko ya papo kwa papo* na *hadithi hutoa mifano ambayo haipo hai wakati sanaa za maonyesho huonyesha vitu ambavyo vipo*. Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.

2 Hadithi ni masimulizi kwa njia ya mdomo yanayo tolewa ili kuelimisha jamii. Na sanaa za maonyesho haya ni mafunzo yanayotolewa kwa njia ya maigizo ili kufikish ujumbe kwa waliokusudiwa. Kwa kutumia hoja tatu za kufanana naeleza kama ifuatavyo:

Zote mbili huwa na fanani na hadhira. ina mana kwamba lazima awepo anayesimulia au kuonyesha na mtazamaji pia au anayesikiliza awepo.

Zote mbili hutumia lugha, ina maana kwamba hadithi na sanaa za maonyesho lazima lugha itumike ili kufikisha ujumbe kwa hadhira waliolengwa kupata ujumbe huo.

Zote lazima ziwe na sehemu ya utendaji, maana yake pawepo na madhari sanaa zote mbili lazima ziwe na sehemu ya utendaji wa kazi hiyo.

Utofauti kati ya Hadithi na sanaa za maonyesho ni kama ifuatavyo:

Hadithi huweza kupokea mabadiliko ya papo kwa papo wakati sanaa za maonyesho haziwezi kupokea mabadiliko ya papo kwa papo kwa mfano, kuuliza swali unapo kuwa unahadithiwa ila kwenye maonyesho si rahi si kuuliza swali.

Hadithi hutoa mifano ambayo haipo hai wakati sanaa za maonyesho huonyesha vitu ambavyo vipo. Kwa mfano hadith walifungwa minyororo ila haionekani ila maonyesho ibaonyesha vitu.


Huo ndio utofauti na ufanano wa hadithi na sanaa za maonyesho kama tanzu za fasihi simulizi.

**Kielelezo Na. 10.1**: Sampuli ya majibu fasaha ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Aidha, watahiniwa 7,311 (35.5%) waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 4 hadi 6. Watahiniwa hao walifafanua kwa usahihi baadhi ya hoja za kufanana na kushindwa kufafanua baadhi ya hoja za kutofautiana kwa tanzu za fasihi simulizi kwa kuwa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu tanzu za fasihi simulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua kwa usahihi kufanana kwa hadithi na sanaa za maonyesho kama vile: *uwepo wa wahusika, uwepo wa mandhari* na

*utendaji* lakini kwa upande wa kutofautisha tanzu hizo alifafanua hoja kama vile: *uwepo wa fani na maudhui* na *lugha* ambazo hazikuwa sahihi hivyo, alipata alama za wastani.

Takwimu zaidi zinaonesha kuwa, watahiniwa 6,557 sawa na asilimia 31.8 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za chini kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kukosa weledi juu ya tanzu za fasihi simulizi. Watahiniwa hao walishindwa kufananisha na kutofautisha tanzu husika na wengine walitoa dhima za hadithi na sanaa za maonesho. Mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja zilizo kinyume kabisa na matakwa ya swali kama vile: *Katika hadithi fanani anasimulia wahusika* lakini katika sanaa *za maonesho wahusika wanavaa uhusika*, *Visa na mikasa ni vya kubuni katika hadithi* lakini katika sanaa za maonesho *ni visa vya kweli, hadithi ni semi fupi hutoa maadili fulani wakati Sanaa za maonyesho ni umbo analotumia msanii kutoa vielelezo vyenye dhana maalum, hadithi husimuliwa karibu na moto wakati sanaa za maonyesho huonyeshwa sehemu mbalimbali, hadithi husimuliwa na bibi au babu lakini sanaa za maonyesho huonyeshwa na mtu anayejua kuchonga vizuri*. Vile vile, alionesha kufanana kwa hizi tanzu mbili kwamba *zote hukuza kazi ya fasihi*. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini.



2. ~~Hadithi~~ Ni kweli kwa hadithi na sanaa za maonyesho hutofautiana - na hufanana kwa hoja zifuatazo,

~~Hadithi~~, kutofautiana.

Hadithi ni usemi fupi unaosimuliwa yenye maneno ya mpangilio ambayo hutoa maadili fulani wakati Sanaa za Maonyesho ni umbo lililosanifiwa umbo ambalo Msanii anaweza kulitumia kwa kutoa kielelezo ~~na~~ au vielelezo zenye dhana maalum.

Hadithi husimuliwa karibu na - moto badala ya kazi hasa wakati wa - jioni lakini sanaa za maonyesho huonyeshwa sehemu mbalimbali.

Hadithi husimuliwa na bibi au babu lakini sanaa za maonyesho - huwa na huonyeshwa na mtu ana yejua kuchonga vizuri.

kufanana -

Hadithi na sanaa ni kazi - ya fasihi simulizi


Hadithi na sanaa na maonyesho ni kukuza kazi ya fasihi.

**Kielelezo Na.10.2**: Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini.

### 3.2.3 Swali la 3: Maendeleo ya Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Maendeleo ya Fasihi simulizi* na lililenga kupima Kumbukumbu na Uelewa. Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja tano kueleza sifa za mtambaji wa fasihi simulizi. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.


Asilimia 98.7 ya watahiniwa ndio waliojibu swali hili. Swali hili lilijibiwa vizuri ambapo asilimia 78.5 ya watahiniwa walifaulu kwa kiwango kizuri na kile cha wastani. Chati Na 11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 11**: *Ufaulu wa Watahiniwa Kiasilimia*

Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 43.2 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama nzuri kuanzia 6 hadi 10 kwa kuwa walitoa hoja tano za kuelezea sifa za mtambaji wa fasihi simulizi.

Miongoni mwao, watahiniwa 2,094 sawa na asilimia 10.2 ya waliojibu swali hili walipata alama za juu kuanzia 8 hadi 10. Hii inaonesha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sifa za mtambaji wa kazi za fasihi simulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alielezea kwa usahihi sifa tano za mtambaji wa fasihi simulizi kama vile: *matumizi ya viungo, matumizi ya ucheshi, atambue utamaduni wa hadhira, atambue aina ya hadhira* na *atumie sauti kubwa.* Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.


3. Mtambaji wa fasihi simulizi ni mtu ambaye anawasilisha simulizi hizo. Mtambaji wa fasihi simulizi anasifa zake. Zifuatazo ni sifa za mtambaji wa kazi ya fasihi simulizi;

Matumizi ya viungo; mtambaji wa fasihi simulizi ni lazima kawe na uwezo wa kutumia viungo vya mwili wake wakati anatoa simulizi ili kuvuta hisia za hadhira.

Matumizi ya ucheshi; pia mtambaji wa kazi ya fasihi simulizi ni lazima atumie ucheshi katika simulizi ili kuipendezesha simulizi yake.

Atambue utamaduni wa hadhira; hii ni sifa nyingine ya mtambaji wa fasihi simulizi ni kuweza kutambua utamaduni wa hadhira anayoenda kuisimulia ili kuepusha migogoro.

Atambue aina ya hadhira; mtambaji wa kazi ya fasihi simulizi ni lazima awe na kutambua aina ya hadhira anayoenda kuisimulia ili kuweza kuelewana na kuepusha migogoro wakati wa simulizi.

Atumie sauti kubwa; lakini pia mtambaji wa kazi ya fasihi simulizi ni lazima atumie sauti inayosikika ili hadhira kuweza kumsikia na kumuelewa.


Hitimisho; endapo mtambaji wa fasihi simulizi hatakosa sifa hizo basi simulizi yake haitoweza kueleweka na hadhira anayoisimulia.

**Kielelezo Na. 11.1**: Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Aidha, asilimia 35.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 4 hadi 6. Hii ni kwasababu waliweza kuelezea kwa usahihi baadhi ya sifa na kushindwa kueleza kwa usahihi sifa nyingine za mtambaji wa fasihi simulizi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza kwa usahihi sifa mbili tu za mtambaji kama vile: (ii) *lazima awe anajua lugha inayotumiwa na hadhira yake* na (iii) *mtambaji wa fasihi simulizi anapaswa awe anajua utamaduni wa jamii au hadhira yake* lakini alielezea sifa za mtambaji zisizo sahihi kama vile; (i) *mtambaji lazima*

*awe anajua matukio mbalimbali yanaleta mafunzo kwa jamii ((*iv*) lazima awe anajua mbinu mbalimbali za kuelimisha, kuburudisha na kuonya jamii* hivyo, mtahiniwa alipata alama za wastani.

Takwimu pia zinaonesha kuwa watahiniwa 7,311 sawa na asilimia 35.5 waliofanya swali hili walipata alama za chini kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kushindwa kabisa kutoa sifa tano za mtambaji wa fasihi simulizi. Baadhi ya watahini walielezea sifa za fasihi simulizi na wengine walielezea dhima za fasihi simulizi kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia dhima za fasihi kama sifa za mtambaji kama vile: *kuelimisha jamii, kuburudisha kuonya jamii, kutunza historia ya jamii* na *ni mali ya jamii nzima* hivyo kupata alama za chini. Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini.



3 Fasihi simulizi ni fasihi inayowasilishwa kwa njia ya masimulizi ya mdomo kwa wasikilizaji. Nathi bitisha kwa hoja tano sifa za fasihi simulizi hapo chini:
Kuelimisha jamii, fasihi huelimisha jamii kwa kuwa mtambaji huwa uwanjani na wasikilizaji hupiga makofi na kushangilia mfano fanani ambaye ndiye Mtambaji jukwaani.
Kuburudisha jamii, fasihi huburudisha jamii kwa kutumia hadithi ngoma na mziki ambayo huwafanya watu wafurahie
Kuonya jamii, kama jamii inaenda kinyume na maadili yaliyowekwa, basi kupitia fasihi watu huonywa mfano kama umetenda kosa ni lazima kuonywa
Kutunza historia ya jamii, fasihi inatunza ~~hito~~ historia kwa wanajamii mfano kuweka kumbu kumbu ~~zot~~ katika kichwa.
Ni mali ya jamii, fasihi ni mali ya jamii kwa sababu ina umri mkubwa na inarithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine
Hivyo basi fasihi ni nguzo muhimu sana kwa maisha ya mwanadamu kwani hukua na hata kufa.

**Kielelezo Na.11.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 3.

### 3.3.2 Swali la 4: Usanifu wa Maandishi

Swali lilitoka katika mada ya *Usanifu wa Maandishi* na lilikuwa mahsusi kupima Uchambuzi. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa afafanue kwa mifano dhahiri vipengele vya kisanaa vilivyotumika katika shairi alilopewa. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilitakiwa kujibiwa na watahiniwa wote 20,784. watahiniwa 20,413 sawa na asilimia 98.2 ndio waliojibu swali hili. Swali hili lilijibiwa vizuri ambapo asilimia 58 ya watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri na wa wastani. Chati Na 12 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 12**: *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Watahiniwa 1,169 sawa na asilimia 11.4 ya watahiniwa 20,413 waliofanya swali walikuwa na ufaulu wa mzuri na kupata alama kuanzia alama 7 hadi 10. Aidha, asilimia 1.5 ya watahiniwa waliofanya swali hili walipata alama za juu zaidi kuanzia alama 8 hadi 10 kutokana na kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vipengele vya kisanaa vilivyotumika katika shairi walilopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alionesha vipengele vya kisanaa kama vile: *mandhari, matumizi ya lugha, muundo, mtindo na mahusika.* Kielelezo Na. 12.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kutokana kukidhi matakwa ya swali.

4. • Aina ya utanzu
Ni ushairi kutokana na mpangilio wa vina na mizani katika beti. hasa kwa upande wa shairi la kimapokeo.

• ~~Muundo~~ Muundo
– Idadi ya mizani.
Mashairi yote yana mizani kumi na sita
mfano ; Napiga mbiu nianga, namwambia wafugao

– Idadi ya beti
Jumla ya beti zipo tano (5)

– Urari wa vina
Mashairi yote ya ~~tat~~ urari wa vina
mfano Nimefikia kituo
wapeni maangalio } kina chake cha kati ni o
sasa watoto ninao

– Idadi ya mistari katika beti
jumla ya mistari katika kila beti iko minne.

– Aina ya kituo ni kituo bahari kwa sababu ni kituo ambacho kinajirudia kila ubeti
mfano : Ng'ombe asiyemchunga, hakosi kutangatanga.

• Mtindo
– Mtindo wa msisitizo
ametumia kituo kuonesha msisitizo
Ng'ombe asiyemchunga, hakosi kutangatanga.

– Mtindo wa masimulizi
Mwandishi anasimulia kuhusu maisha ya wafugaji na kuwaambia wanatakiwa wafuge vizuri mifugo yao

• Wahusika
– Ng'ombe
Anamaanisha watoto wanatakiwa kuchungwa na kufundishwa maadili mema.
– Wafugaji
Anamaanisha wazazi wanatakiwa kuwaleo watoto wao katika maadili mema.
– Watoto
wanaaswa kutulia kwa wazazi wao na kujiepusha na mambo mabaya

• Mandhari.
– Mandhari ya kijijini.
mfano : Ng'ombe maziwa mwao

• Matumizi ya lugha
– Aina ya lugha iliyotumika ni changamano, nyepesi na ngumu
Matumizi ya semi.
– Nahau
• Ng'ombe usiyemchunga hakosi kutangatanga.
• Naha ranga.
Tamathali za semi
– ~~Wa~~ Sitiari
– Wapeni mikomamanga.
• Mubalagha
Mbinu nyingine za kisanaa
– Takriri
– Ng'ombe

**Kielelezo Na. 12.1**: Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Aidha, takwimu zinaonesha kuwa, watahiniwa 20,413 sawa na asilimia 46.7 ya waliofanya mtihani huu walipata alama za wastani kuanzia 4 hadi 6. Ufaulu huu kulitokana na walitakiwa kufafanua kwa usahihi baadhi ya vipengele na kushindwa kufafanua vipengele vingine vya kisanaa katika shairi walilopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua kwa usahihi vipengele kama vile: *wahusika, mandhari, matumizi ya taswira na muundo.* Katika muundo, aliweza kufafanua kipengele kimoja cha *idadi ya mistari minne* na kushindwa kufafanua vipengele vya *mshororo* na *mstari wa kituo* ambao unajirudiarudia katika kila ubeti. Vile vile, alifafanua kwa usahihi kipengele kimoja tu cha *taswira* hivyo, alipata alama za wastani.

Takwimu zaidi zinaonesha kuwa watahiniwa 2,892 sawa na asilimia 41.9 walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 3 kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Usanifu wa Maandishi. Watahiniwa hao walishindwa kubaini vipengele vingi vya kisanaa vilivyotumika katika shairi walilopewa na wengine waliandika ufupisho wa shairi kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama vile: *muundo na mtindo*. Mtahiniwa huyu alifafanua miundo inayotumika katika riwaya na tamthiliya na sio katika shairi alilopewa, katika kipengele cha *matumizi ya lugha.* Mtahiniwa alifafanua *mtindo, matumizi ya lugha tamathali za semi*, *tashibiha* na *sitiari* kinyume na yalivyotumika katika shairi alilopewa, lakini aliweza kufafanua kwa usahihi vipengele vya *wahusika* na *mandhari*. Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini.

4 Usanifu wa mwandishi: ni dhana inayotumia vipengele mbalimbali vilivyoweza kufikisha ujumbe kwa jamii kupitia muundo, mtindo, mandhari na wahusika pia usanifu wa mwandishi ni kipengele cha habari, shairi, ngonjera. Vipengele vya usanifu vilivyotumika katika shairi:

Muundo: ni mpangilio wa vina na mizani katika kazi ya sanaa mwandishi ametumia muundo wa moja kwa moja anasema mwandishi "... Napiga mbiu kiranga, namwambia watu ugao ..."

Mtindo: ni mpangilio ambao unaonyesha tofauti zilizopo kati ya mwandishi mmoja na mwingine katika shairi mwandishi ametumia mtindo mbalimbali yani:


mtindo wa masimulizi: ambapo tunaona mwandishi anawasimulia wafugaji anasema "...Ngombe mazizini mwao, wengi wanawafunga ..."

mtindo wa majibizano: hapa tunamuona mwandishi anajibizana wao kwa wao anaposema "... Lawa ya ngombe mchunga, Mchunga ndo dawa yao ..."

Wahusika: hapa mwandishi ametumia wahusika wawili yani ngombe na watoto anaposema. "... Ngombe mazizi mwao ..." Pia "... Watoto ninao wangu mie namchunga ...

Mandhari: mwandishi ameonyesha mandhari ya Mazizi anaposema "...Ngombe mazizi mwao, wengi wanawafunga ..."

Matumizi ya lugha: ni hali ya kutumia sanaa au fasihi kuweza kufikisha ujumbe ulio kusudiwa katika jamii.


4 Lugha ni sauti za nasibu zenye kubeba maana ambayo imekubalika ili kuwasiliana.
Tamathali za semi ni vipengele mbalimbali ambavyo utumika katika kupitisha ujumbe kwenye jamii. huvitika vifuatavyo ni vipengele vya tamatathali za semi
Tashibiha ni aina ya tamathali za semi ambazo zinaunganisho vitu viwili kwa wakati mmoja mfano mwandishi anavyosema "... na kuwaweka kitao, kwa kutuso kuwachunga ..."
Sitiari ni alama ambayo inatumika kuonyesha msisitizo wa maneno katika fasihi mwandishi anasema "... Ng'ombe asiyemchunga, hakosi kutangatanga ..."
Hivyo basi mwandishi amptumia hadhira wake mbalimbali ili kuweza kupitisha ujumbe kwa jamii kupitia vipengele mbalimba vya kisanaa.

**Kielelezo Na.12.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 4.


## 3.3 SEHEMU B

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) ya insha. Mtahiniwa alitakiwa kujibu swali la tano na maswali mawili zaidi. Sehemu hii ilikuwa na jumla ya alama 60 na kila swali lilikuwa na alama 20.

### 3.3.1 Swali la 5: Uhakiki wa Ushairi

Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi*, mada ndogo ya *uhakiki wa Ushairi*. Swali lilikuwa mahsusi kwa ajili ya kupima Tathmini. Katika swali hili mtahiniwa alitakiwa kubainisha mafunzo yanayotolewa na washairi kwa jamii kwa kutoa hoja nne kwa kila kitabu kutoka katika diwani mbili alizosoma.

Takwimu zinaonesha kuwa watahiniwa wote 20,784 walifanya swali hili. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo asilimia 99.3 walipata alama za wastani na zaidi kuanzia 12 hadi 20. Chati Na.13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika asilimia.




**Chati Na.13**: *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa swali hili lilijibiwa vizuri sana na watahiniwa wengi. Watahiniwa 17,456 walikuwa na ufaulu mzuri kuanzia alama 12 hadi 20 kwa kuwa waliweza kubainisha mafunzo yanayotolewa na washairi kwa jamii. Miongoni mwao, watahiniwa 1,088 sawa na asilimia 0.6 walijibu vizuri zaidi na kupata alama za juu kuanzia 18 hadi 20. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu vizuri swali hili ambapo katika diwani ya *Mapenzi Bora* alibainisha mafunzo kama vile: *uwepo wa mapenzi bora ni chanzo cha ukombozi, kukosekana kwa mapenzi bora husababisha ubaguzi, wizi ni chanzo cha kushuka kwa maendeleo, uzalendo ni chanzo cha kulinda amani ya nchi, mapenzi bora huondoa chuki* na *kukosekana kwa mapenzi bora ni chanzo cha uchoyo*, katika diwani ya *Fungate ya Uhuru* alibainisha mafunzo kama vile: *uongozi mbaya ni chanzo cha uhujumu uchumi* na *kupiga vita matabaka husaidia kujenga jamii mpya*. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu kutokana na kutoa majibu yaliyokidhi matakwa ya swali.

5. Mafunzo ni ujumbe unaotolewa na waandishi ili jamii iweze kujifunza mazuri na kuacha mabaya. Washairi ni wale wanaotunga mashairi ~~kwa~~ lengo la kuwadilisha wale. Diwani ya "~~Kimbunga~~ Fungate ya uhuru" ya ~~Haji Gora~~ S. Khatib na Utenzi wa MAPENZI BORA wa SHAABAN ROBERT wameonesha mafunzo mbali mbali kwa jamii. Kwa kuanza na Utenzi wa "Mapenzi bora" yafuatayo ni mafunzo kwa jamii:

Uwepo wa mapenzi bora ni chanzo cha Ukombozi ni funzo lililotolewa na Mshairi, Shaaban Robert ameonesha faida ya kuwa na mapenzi bora ambayo hupelekea ukombozi katika jamii kwa sababu wale huweza kuungana, kwa mfano Malenga anathibitisha hilo kupitia ubeti ufuatao:

"- - - - - - - -
Mapenzi wanahitaji,
Wale kama ukombozi."

hivyo wanajamii tunaonywa ili tupate ukombozi ni lazima tuwe na mapenzi bora kati yetu wenyewe.

Kukosekana kwa mapenzi bora husababisha ubaguzi ni funzo lililotolewa na Msanii Malenga ameonesha ~~chuki~~ ubaguzi kwa mataifo mbali mbali ambayo imesababishwa na ubaguzi wa rangi, sifa na hadhi, kwa mfano wa Ulaya, Marekani na Asia pamoja na Afrika kuna ubaguzi mkubwa, Mfano ubeti ufuatao:

"Mapenzi wanayo mengi,
Binadamu kila rangi,
lakini hayawaungi,
kwa sera ya ubaguzi."

Mshairi anetoa funzo hili ili wanajamii tuwe na mapenzi bora ili tuondoe ubaguzi kwani unasababisha kutoweka kwa amani.

Mapenzi bora huondoa chuki ni funzo lililotokana na Msanii, chuki imeota mizizi katika jamii zetu ambapo wale huchukiana, Shaaban Robert ameonesha hilo kwa ~~kuwa~~ chuki husababisha wale kutoungana, Mfano anathibitisha hilo katika ubeti ufuatao:

"Chuki madhara ya dhati,
~~Afa~~ dhali ya umauti,
~~tat~~ ni faradhi kwa umati,
chuki inanyong'o nyezi."

hivyo wanajamii tuwe na mapenzi bora ili chuki kati yetu iyondoke kwani ni ~~kwazo~~ kikwazo cha maendeleo.


Kukosekana kwa mapenzi bora ni chanzo cha kuwepo kwa uchoyo ni funzo la msanii, hii ni hali ya ubinafsi wa mtu kutosaidia wengine, Shaaban Robert ameeleza hali ya uchoyo kusasa kutokana na kutoweka kwa mapenzi, mfano anasema;

"Akijua katika choyo,
Mtu fahamu hanayo,
kadri ya hali iwayo,

**Kielelezo Na.13.1**: Sampuli ya sehemu ya majibu fasaha ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Aidha, asilimia 15.3 ya watahiniwa walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kwa sababu walishindwa kutoa maelezo sahihi kwa baadhi ya mafunzo yanayotolewa na washairi, wengine walichanganya mashairi ya diwani moja na nyingine na wengine waliandika vibaya majina ya mashairi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya mashairi ya *Fungate ya uhuru* na ya *Kimbunga*. Mfano: shairi la *Vijana wa Zanzibari, Paka* na *Wenye vyao watubana* ambayo hayamo kwenye diwani ya *Fungate ya Uhuru* bali yamo kwenye diwani ya *Kimbunga* lakini baadhi ya mashairi aliyakosea majina ambayo ni *Vijana wa Zanzibari* na *Wenye vyao* badala ya *Vijana wa Zanzibar* na *Wenye vyao Watubana* hivyo, alipata alama za wastani.

Watahiniwa 148 sawa na asilimia 0.7 ya watahiniwa wote walipata alama za chini kuanzia 0 hadi 6.5. Hii inaonesha kuwa hawakuwa na ujuzi wa mada ya *uhakiki wa ushairi* na kutoelewa madai ya swali. Wengi wao walijibu kwa kuonesha vipengele vya fani hasa matumizi ya lugha kutoka katika vitabu na wengine walijadili dhamira za vitabu bila kuzingatia matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alibainisha majibu kama vile: u*muhimu wa mapenzi bora, aina ya mapenzi, athari za mapenzi, umuhimu wa kuheshimiana* na *namna au mbinu za kulinda mapenzi bora* na katika diwani ya *Chungu Tamu* alibainisha dhamira kama vile: *mambo yanayosababisha matabaka, rushwa* na *matabaka* badala ya kubainisha mafunzo yanayotolewa na washairi katika jamii hivyo, alipata alama za chini. Kielelezo Na. 13.2 ni sampuli ya sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za chini.



5 Funzo au maadili ni ule ujumbe unaoupata baada ya kusoma kazi za fasihi, katika Diwani wa Mapenzi bora na Chungu tamu washairi wameiadilisha jamii kwa kuonesha au kutoa mafunzo mbalimbali kwa jamii. Mafunzo hayo ni kama ya fuatayo:

Umuhimu wa mapenzi bora; Shaaban :- katika diwani hii amefafanua umuhimu wa mapenzi bora na maana ya mapenzi bora amesema mapenzi bora ni yale Mungu kutupenda katika ubeti wa 122 anasema, mapenzi apewe - mungu.

Aina ya mapenzi; Mwandishi Shaaban - ametufafanulia aina mbalimbali za mapenzi - amejadili suali hili kwa mapana na kusema kuwa kuna aina nyingi za mapenzi, lakini kwa mujibu wa kazi yake hii anatuhitimishia kwa kusema mapenzi bora ni yale ya mungu tu zingine zote ni kawaida tu -

Umuhimu wa kuheshimiana; mwandishi wa diwani ya mapenzi bora ameweka bayana umuhimu wa kuheshimiana katika jamii pale ambapo amesema kuheshimiana na ishara ya kupendana na mtu asipompenda ndugu yake hawezi kumpenda mungu. hivyo upendo ni heshima kwetu sisi wanadamu.

Namna au mbinu za kulinda mapenzi - bora, mwandishi amezungumzia suala hili - na kutuweka bayana ubayana wake ya - kuwa mapenzi ni muhimu yakikosekana - ina athari kubwa katika jamii hivyo - amewasihi jamii wazingatie kanuni bora za kulinda mapenzi yaliyobora, vilevile katika Diwani Chungu tamu iliyo andikwa na Theobald mvungi mwandishi ametoa ujumbe ufuatao:-

Athari za matabaka; mwandishi wa diwani ya Chungu tamu katika shairi la chatu na kuku ame onesha athari zitokanazo na - matabaka yaani tabaka lawala na tabaka lawaliwa mwandishi amesema kuwa - katika jamii suala la matatabaka huleta athari kubwa hivyo tuepuke matabaka katika jamii

Mambo yanayosababisha matabaka; - Mwandishi Theobaldi amezungumzia juu ya visabishi vya rushwa kwa kusema - kuwa matabaka husababishwa na mfumo wa utawala hivyo jamii inaaswa itazame kwa makini mfumo wake wa uongozi kama unasababisha matabaka kutokea.

Rushwa; Mwandishi Theobaldi mvungi ametupa funzo juu ya chanzo cha rushwa katika shairi la "Chini ya mti mkavu" shairi hili kwa ujumla limezungumzia - suala la rushwa na kuiasa jamii iwe - makini katika kupambana na rushwa - kama ilivyo kilwaro katika Ujenzi wa - Taifa


Matabaka ni chanzo cha umaskini mwandishi ametukumbusha katika shairi la "Chini ya mti mkavu" anatutahadharisha kuwa jamii iondokane na matabaka ili kujenga jamii yenye kujali maslahi ya wote.

**Kielelezo Na.13.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi katika swali la 5.

### 3.3.2 Swali la 6: Uhakiki wa Ushairi

Takwimu za uchambuzi zinaonesha kuwa, swali lilitoka katika mada ya Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi, mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi*. Swali liliandaliwa mahsusi kwa kupima Tathmini na lilimtaka mtahiniwa kueleza umuhimu wa kipengele cha lugha kwa mtunzi wa shairi ili kumuwezesha msomaji kupata ujumbe uliokusudiwa katika diwani mbili alizosoma kwa kutumia hoja tatu kwa kila diwani. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Watahiniwa 17,420 sawa na asilimia 83.8 walijibu swali hili kwa kuwa lilikuwa la kuchagua. Miongoni mwao asilimia 73.2 walikuwa na ufaulu wa kiwango kizuri na kile cha wastani. Chati Na. 14 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na 14**: *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia*


Watahiniwa 6,703 sawa na asilimia 38.5 ya waliojibu swali hili walipata alama nzuri kuanzia 12 hadi 19. Kati yao, watahiniwa 8 walipata alama za juu kuanzia 18 hadi 19 kwa kuwa walielewa mada ya ushairi na kuweza kuelezea umuhimu wa kipengele cha lugha katika shairi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutaja na kuelezea ipasavyo vipengele vya lugha kama vile: *misemo*, *taswira*, *tashibiha*, *tashihisi* na *tafsida*. Kielelezo Na. 14.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu kwa usahihi swali hili na kupata alama za juu.

06 Lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zenye
kubeba maana zilizokubaliwa na jamii ya watu
fulani zitumike kuwasiliana miongoni mwao. Niku
li mtunzi wa shairi hutumia kipengele cha lugha ili
kumwezesha msomaji kupata ujumbe uliokusudiwa. Nita
tumia diwani mbili nilizosoma kuonyesha namna
watunzi wa ushairi walivyotumia kipengele cha lugha
kufikisha ujumbe ambazo ni "FUNGATE YA UHU
RU" ya mwandishi Mohammed S Khatibu na "CHUNGU
TAMU" ya mwandishi Theobald A. Mvungi. Nikianza
na diwani ya "FUNGATE YA UHURU" :-

Misemo, mwandishi wa diwani hii ameti
mia misemo kama kipengele cha lugha kufikisha uju
mbe kwa jamii kwa mfano "paka shume" ametumi
kuonesha wezi wa mali za umma katika jamii katika
shairi la "paka shume" uk 45, pia msemo mwingine ni
"Joka la mdimu" kuashiria jambo lenye kuleta madhara
na malumbwa katika jamii mfano, ukoloni mamboleo
katika shairi la "Joka la mdimu" uk 40.

Tashibiha, pia mwandishi ametumia mbinu
hii kama kipengele cha lugha kufikisha ujumbe kwa
jamii mfano wa Tashibiha ni kama vile "Kitanda
nikilala ni kama dema la varaki" katika shairi
la "mkata". Ametumia kuonesha hali ngumu ya mai
sha.

Taswira (Lugha ya picha), pia mwandishi
ametumia taswira mbalimbali kufikisha ujumbe kama
vile "Mjamzito" ~~akimaanisha~~ ~~kwa~~ kuwakilisha
viongozi waoga ambao wanashindwa kutimiza wajibu
wao kwa raia katika shairi la "Mjamzito", pia
taswira nyingine ni "Nahodha mtwesi" ambayo inaw
akilisha viongozi bora katika shairi la "Nahodha mtwesi"



06 Pia mwandishi wa diwani ya "Chungu Tamu" ametumia kipengele cha lugha ili kumwezesha msomaji kupata ujumbe uliokusudiwa kama ifuatavyo:-

Tashihisi, mwandishi ametumia mbinu hii kwa kuvipa vitu visivyoona uwezo wa kutenda kutenda kama kama binadamu, Mfano wa Tashihisi iliyotumiwa na mwandishi ni "Tabu imekuradaki" katika shairi la "wanajua kuvumilia" akimaanisha kuwa watu wa tabaka la chini wanavyonyaswa na tabaka tawala.

Taftida, mwandishi pia amelitumia taftida kama kipengele cha lugha kufikisha ujumbe kwa jamii kwa kupunguza ukali wa maneno, mfano, wa taftida alizotumia mwandishi ni kama ile "Nampendelea sana" katika shairi la "Fikra za waungwana" akionesha namna ambavyo mhusika Anna alivyokuwa anampendelea Joseph kwa kufanya nayo ngono.

Taswira (Lugha ya picha), mwandishi ametumia taswira mbalimbali kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii mfano. "Noulu" ametumia kuonesha ukhamu za viongozi zilizosahaulika na kutaka watu wathamini kuwa wanapotoka katika shairi la "Noulu wapaona", pia taswira nyingine ni "radi" ambayo ametumia kuashiria njaa na athari zake katika shairi la "radi ya kiangazi"

Kimsingi, watunzi wa ushairi pia huandika kazi zao kutokana na msukumo wa mambo mbalimbali yanayotokana na jamii zao kama vile usaliti na kutoa matumizi mbalimbali kama vile umuhimu wa kupinga vita usaliti.

**Kielelezo Na. 14.1**: Sampuli ya majibu fasaha ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Hata hivyo, watahiniwa 6,048 sawa na asilimia 34.7 ya waliojibu swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 baada ya kuelezea kwa usahihi baadhi ya vipengele vya lugha na kushindwa kuelezea vipengele vingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya *Chungu Tamu* alielezea vipengele kama vile: *tabaini*, *tashibiha*, *taswira* na *takriri* lakini katika mifano ya majibu yake alionesha kuwa usaliti na dhuluma ni chachu ya maendeleo kitu ambacho si kweli na katika diwani ya *Kimbunga* alielezea vipengele kama vile: *tashihisi*, *tashibiha* na *taswira* lakini alishindwa kabisa kuielezea taswira hivyo, alipata alama za wastani.

Vile vile, watahiniwa 4,669 sawa na asilimia 26.8 ya waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kuwa na uelewa mdogo wa mada ya *Uhakiki wa Ushairi* hasa katika kipengele cha lugha. Watahiniwa hao walitoa majibu ambayo yalikuwa ni kinyume kabisa na matakwa ya swali. Pia, watahiniwa wengine walitoa dhamira mbalimbali

za vitabu na wengine walionesha kufaulu na kutofaulu kwa wasanii katika kipengele cha lugha kinyume kabisa na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika diwani ya *Kimbunga na Mapenzi Bora* alielezea mambo tofauti na mahitaji ya swali kama vile: *kutambua usawa wa urari na vina katika shairi, kuweza kufuata alama za uandishi kuweza kutumia msamiati, kufahamu maana ya misemo, nahau na methali, Kuweza kuimbika kwa shairi* na *humsaidia mtunzi kuweza kutumia mkato wa maneno, leseni ya ushairi.* Vile vile utangulizi na hitimisho lake havikuendana na swali. Kielelezo Na.14.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali na kupata alama za chini.


uliokusudiwa kama ifuatavyo;
Kutambua usawa wa urari na vina katika sh
airi, ili mtunzi wa shairi aweze kueleweka vizuri nilazim
a atambua usawa wa urari na vina katika shairi lake
na hivyo kuweza kumfanya msomaji aweze kuelewa vi
zuri maana ya maneno yaliyotumika.
Kuweza kufuata alama za uandishi, Pia
ili mtunzi wa shairi aweze kueleweka kwa msomaji
ni lazima kufuata alama za uandishi mfano mkato,
nukta na funga semi na fungua semi.
Kuweza kutumia msamiati, Pia mtunzi
wa shairi hanabudi kuzingatia msamiati katika shairi
ili kuweza kueleweka kwa msomaji wa shairi, msa
miati ukitumika sehemu husika humuwezesha msomaj
i kuelewa makusudio ya msamiati huo.
Kwa kutumia diwani ya Mapenzi Bora
na SHABANI ROBERT, mtunzi wa shairi lazima kuzing
atia kipengele cha lugha ili;
Kufahamu maana ya misemo, Nahau na
methali, Endapo mtunzi atakua ametumia Nahau, m
isemo na methali nirahisi kueleweka kwa msomaji
huyo, kitumike kimoja kimoja sio kuchanganya vyote mf
ano Mwandishi wa Mapenzi bora ametumia misemo kama
aliepo nyumbani, fungu langu.
Kuweza kuimbika kwa shairi; vilevile
mtunzi wa shairi lazima kuzingatia shairi lenye m
vuto wa kuimbika kwa maana azingatie kilio katika
shairi au kibwagizo.
Humsaidia mtunzi kuweza kutumia mkato
wa maneno, leseni ya ushairi, kipengele cha lugha humu
wezesha mtunzi wa shairi kuweza kupachika maneno
ambapo anaona litafaa kukaa bila kujali neno limeka
aa au mfano neno b'shara badala ya biashara mtu
nzi humsaidia katika kuandaa shairi lake kwa utaratibu
mzuri na unaoeleweka kwa msomaji.
Hivyobasi, kipengele cha lugha kina mambo
kadhaa mfano, Tashtiti, Takriri, Tashihisi, Taraza kali sa
udi, Tafsida, Mubalagha na sitiari. hivi humsaidia mtu
nzi wa shairi kuitumia sehemu anayoona itakua na
umuhimu wa kuiweka ili kuleta maana na kumuwezesha
msomaji kupata ujumbe uliokusudiwa.

**Kielelezo Na. 14.2:** Sampuli yasiyosahihi katika swali la 6.

### 3.3.3 Swali la 7 Uhakiki wa Riwaya

Swali lilitoka kwenye mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi andishi* na lilihusu *uhakiki wa riwaya*. Swali lilikuwa mahsusi kupima Tathmini na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kauli isemayo, ‘‘Mwandishi wa fasihi ni chachu ya mabadiliko chanya katika jamii ili kuwa na maisha bora’’ kwa kutumia riwaya mbili alizosoma na kutoa hoja nne kwa kila kitabu. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili lilijibiwa vizuri na watahiniwa wengi (20,731) ambao ni sawa na asilimia 99.7 ya watahiniwa waliofanya mtihani huu. Kiwango cha ufaulu kilikuwa kizuri ambapo, asilimia 99.4 ya waliojibu swali hili walipata alama nzuri na zile za wastani. Chati Na 15 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kiasilimia.




**Chati Na 15:** *Ufaulu wa Watahiniwa Kiasilimia*

Uchambuzi unaonesha kuwa, asilimia 90.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walifaulu vizuri kwa kupata alama 12 hadi 20. Miongoni mwao, watahiniwa 422 (02%) walipata alama za juu kuanzia 18 hadi 20 kutokana na kujibu kulingana na matakwa ya swali. Watahiniwa hao walitoa hoja nne sahihi kwa kila kitabu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitumia riwaya ya *Vuta N’kuvute* kutoa hoja kama vile: *harakati za kupigana, uongozi usiofaa* na *umuhimu wa mwanamke katika jamii* na katika riwaya ya *Usiku Utakapokwisha* alitoa hoja kama vile: *Kukosoa wizi na ujambazi* na *kupinga matabaka katika jamii* na kisha alitoa ufafanuzi unaojitosheleza kuthibitisha majibu yake. Kielelezo Na. 15.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili.

7 Mwandishi wa fasihi ni chachu ya mabadiliko chanya katika jamii ili kuwa na maisha bora. Thibitisha kauli hiyo kwa kutumia riwaya mbili.

Fasihi ni kazi ya sanaa ambayo inahusisha lugha katika kufikisha habari kwa jamii. Mwandishi wa fasihi ni mtu anayejihusisha na utunzi wa kazi za fasihi. Katika jamii wanafasihi wamekuwa ni mchango mkubwa sana katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii ambapo michango hiyo husaidia kuwepo kwa maisha bora katika jamii. Kwa kutumia riwaya ya Usiku utakapokwisha, iliyoandikwa na Mbunda Msokile na riwaya ya Vuta N'kuvute, iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi kuonyesha jinsi waandishi wa fasihi walivyo chachu katika mabadiliko chanya ya jamii.

Kwa kuanza na riwaya ya Vuta N'kuvute, iliyoandikwa na mtunzi Shafi Adam Shafi kuonyesha jinsi mwandishi alivyofanikiwa kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Kuonyesha ukombozi wa jamii, Shafi Adam Shafi moja kati ya juhudi yake katika kuleta mabadiliko chanya katika jamii ni kuonyesha ukombozi katika jamii ambapo katika riwaya ameweza kuonyesha ukombozi wa jamii kutokana na mila na desturi potofu kwa mfano familia ya Yasmini ilipomlazimisha binti yao aolewe na mwanaume asiyempenda ambapo ni moja kati ya mila na desturi zilizopitwa na wakati.

Kuonyesha ubaguzi wa rangi, pia mwandishi Shafi Adam Shafi pia ameonyesha viashiria vya ubaguzi wa rangi na kuupinga kutokana na kuwa ubaguzi wa rangi huchangia kutokuwepo kwa usawa katika

**Kielelezo Na. 15.1**: Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Hata hivyo, watahiniwa 1,876 (09%) ya waliofanya swali hili walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa maelezo ambayo baadhi yalijitosheleza na mengine hayakujitosheleza kujibu swali. Baadhi ya watahiniwa walitoa ujumbe wa wasanii na wengine walionesha sifa mbalimbali za wahusika katika tamthiliya kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja katika riwaya ya *Mfadhili* alitoa majibu kama vile: *usanifishaji haukushirikisha wenyeji na kutokubalika kwa lahaja ya kiunguja lakini alishindwa kutoa maelezo yaliyojitosheleza* kwani hoja hazikuonesha ni kwa namna gani ni chachu ya mabadiliko chanya ya jamii. Lakini katika riwaya ya *Kufikirika* mtahiniwa alieleza kwa usahihi mambo kama vile: *umoja ni nguvu utengano ni dhaifu, uongozi bora huleta maendeleo, elimu ni ufunguo wa maisha* lakini hoja ya *mwisho ni vizuri kuwaenzi mashujaa* maelezo yake hayakujitosheleza hivyo, akapata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa wachache (120) sawa na asilimia 0.6 ya waliojibu swali hili na wakapata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo juu ya mada ya uhakiki wa riwaya, watahiniwa wengine walielezea ujumbe wa wasanii katika vitabu na wengine walielezea dhamira hasi hivyo, walishindwa kuthibitisha namna gani fasihi ni chachu ya mabadiliko chanya katika jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile: *uongozi bora, mapenzi na ndoa , usaliti, athari za ulevi, mila na desturi potofu, wivu katika ndoa, upendo wa kweli* na *mivutano katika jamii juu ya ukale na usasa* lakini katika maelezo ya hoja zote alichanganya majina ya wahusika katika riwaya hizo mfano, muhusika *Yasmin* aliwekwa katika riwaya ya *Mfadhili* badala ya riwaya ya *Vuta N'kuvute*. Vile vile ufafanuzi katika hoja zote haukujitosheleza kujibu swali. Kielelezo Na. 15.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyefanya vibaya swali hili na kupata alama za chini.

7. Ipo wazi hata katika jamii zetu, ndoa nyingi zime vunjika na wengine hata maafa kutokana na wivu.

Upendo wa kweli, hapa msanii amemtumia Mwajuma kuwa na mapenzi ya dhati kwa Dania na kumhifadhi aliyotoroka kwa Shihabu pia Bukheti alikuwa na mapenzi ya kweli kwa Dania kivyo jamii yifunze kuwa akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki

Mivutano katika jamii juu ya ukale na usasa hapa msanii amefafanua kwa kutumia familia ya Dania na jamii yake ambaye ilikuwa imeshikilia masuala ya kale ambapo na vyara wakitaka kubadili kulingana na wakati mfano ndoa za kulazimisha, kuweka wanawake utawani, kumchagulia mtu mwenzi, kuzingatia kabila, rangi katika ndoa ambapo yote haya yamepitwa na wakati

Kutoka na hoja zote hapo juu kutoka katika riwaya zote mbili wasanii wamekuwa wakielimisha jamii ili kuweza kujenga jamii mpya yenye mtazamo chanya, kuelimisha juu ya rushwa, wizi, utapeli, madhara yake pamoja na kupendelekeza njia za kujikwamua kiuchumi kama kujituma katika kazi na kuwashirikisha wanawake maana wanaweza


Ushairi ni kazi ya fasihi inayowasilishwa kwa njia ya maandishi iliyobeba lugha yenye ujazo, pia huambatana na vitendo katika uwasilishaji wake, kuna aina mbili za mashairi ambazo ni Ushairi wa kimapokeo, wenye ulali wa vina na mizani na Ushairi wa kisasa usiozingatia ulali wa vina na mizani, lakini aina zote hutumia lugha zenye mjazo.

**Kielelezo 15.2**: Sampuli ya majibu yasiyoridhisha katika swali la 7.

### 3.3.4 Swali la 8: Uhakiki wa Tamthiliya


Swali lilitoka katika mada ya Uhakiki wa Kazi za Fasihi Andishi katika mada ndogo ya Uhakiki wa Tamthiliya. Swali lililenga kupima Tathmini na lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha hoja inayosema ‘‘Fasihi andishi ya Kiswahili ni kapu kubwa lililosheheni semi’’ kwa kutumia misemo mitatu, methali tatu na nahau tatu kwa kila kitabu katika tamthiliya mbili alizosoma, aoneshe lengo la mwandishi katika kutumia semi hizo. Swali lilikuwa na jumla ya alama 20.

Swali hili ndilo lililojibiwa na watahiniwa wachache zaidi (2,738) ambao ni sawa na asilimia 13.2 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huu. Miongoni mwao, watahiniwa wengi (63.7%) walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu wa kupata alama kuanzia 0 hadi 6.5. Chati Na 16 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika asilimia.




**Chati Na 16:** *Ufaulu wa Watahiniwa Kiasilimia*


Watahiniwa 265 sawa na asilimia 9.7 walipata alama nzuri kuanzia 12 hadi 18.5. Kati yao, watahiniwa 3 walipata alama za juu kuanzia 18 hadi 18.5 kwa kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha juu ya matumizi ya semi katika utanzu wa tamthiliya. Watahiniwa hao, waliweza kutoa misemo sahihi kama vile; *mie breki mie jeki kwangu utasimama, bei zenyewe zinaruka* na *heri hupatikana ndani ya tumbo la shari*. Kielelezo Na. 16.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.



**Kielelezo Na. 16.1**: Sampuli ya majibu fasaha ya mtahiniwa aliyepata alama za juu.

Aidha, watahiniwa 729 sawa na asilimia 26.6 walipata alama za wastani kuanzia 7 hadi 11.5 kutokana na kutoa majibu yasiyojitosheleza kwa baadhi ya semi. Watahiniwa hawa, waliweza kuthibitisha kwa usahihi baadhi ya semi na kushindwa kueleza kwa usahihi semi nyingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliweza kutaja misemo mitatu katika tamthiliya ya Nguzo Mama kama vile: *umeshindwa kumtunza kaja kwangu*, *Anajifanya mjuaji* na *Huna mbele wala nyuma*, methali tatu: *Pilipili usiyoila yakuwashia nini*, *Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu* na *kidole kimoja hakivunji chawa* na nahau mbili: *asiejua maana haambiwi maana* na *elimu haina mwisho*. Katika tamthiliya ya *Morani* alitoa misemo kama, *kula bata, wajinga ndio waliwao na maisha yenyewe ndo haya*; methali tatu: *umoja ni nguvu* na *utengano ni udhaifu*, *kikulacho ki nguoni mwako* na *mwosha huoshwa* na nahau mbili: *adhabu ya kaburi ajuaye maiti* na *mchimba kisima hudumbukia mwenyewe* kuthibitisha hoja hiyo lakini katika maelezo yake yalishindwa kuonesha lengo la mwandishi katika kutumia semi hizo hivyo, akapata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa 1,744 ya waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 6.5 kutokana na kukosa uelewa wa mada na kutozingatia matakawa ya swali. Watahiniwa wengi walishindwa kutofautisha nahau, methali na misemo. Pia, walielezea dhamira na tamathali za semi kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama vile: *tafsida, matumizi ya nyimbo, matumizi ya vitendawili* na *mbalaga* ambavyo ni vipengele vya matumizi ya lugha kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo Na. 16.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetoa nahau, misemo na methali katika kujibu swali badala yake alitoa tashihisi, mdahizo na tashibiha akidhani ni nahau, misemo na methali na kupata alama za chini.



08 [illegible]
[illegible]
Semi ni kipengele moja wapo cha fani katika kufikisha ujumbe katika jamii husika ambapo huweza mara kuchora tofauti tofauti kama ifuatavyo.
Tashihisi hizi ni semi ambazo hujitokeza katika kazi ya fasihi kutoka kipengele cha semi.
Mdokezo pia hizi ni semi ambazo hujitokeza katika utunzi wa fani katika uchambuzi wa kazi ya fasihi.
Tashibiha hizi ni aina ya semi ambazo hujitokeza katika kazi ya fasihi ili kufikisha ujumbe ulio kusudiwa na hisia tofauti tofauti zilizo katika kazi ya fasihi
Tafsida pia ni usemi unao tumika katika kazi ya fasihi ili kufikisha ujumbe ulio kusudiwa katika jamii husika
Matumizi ya nyimbo pia hizi ni semi ambazo hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi ili kufikisha ujumbe katika jamii
Matumizi ya vitendawili pia hii ni aina ya semi ambazo hujitokeza katika kazi za fasihi
Methali hii pia ni aina ya semi ambazo hujitokeza katika kazi za fani ili kufikisha ujumbe

**Kielelezo Na. 16.2**: Sampuli ya majibu yasiyosahihi ya mtahiniwa katika swali la 8.

## 4.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA

Uchambuzi wa takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili unaonesha kuwa, watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika mada zote kumi na moja (11).

Ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2020 ikilinganishwa na ule wa mwaka 2019 umeongezeka katika mada zifuatazo: *Ufahamu na ufupisho (99.6%), Matumizi ya Sarufi (95.8), Utumizi wa Lugha (95%) na ushairi (86.3%).* Kwa mwaka 2019, ufaulu wa watahiniwa katika mada hizo ulikuwa ni wa chini ambapo, *Ufahamu na ufupisho (97.8%), Matumizi ya sarufi (82.1%), Utumizi wa Lugha (76.2%) na ushairi (75.2%).*

Aidha, ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2020 umepungua katika mada za *Tafsiri na Ukalimani* (69.7%), *Tamthiliya* (36.5%), Utungaji (97.2%), *Usanifu wa Maandishi* (58%*) na Fasihi kwa Ujumla* (70.2%). ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo kiwango cha ufaulu wa mada kilikuwa *Tafsiri na Ukalimani* (99.6%), *Tamthiliya* (99.3%), Utungaji (98.3%), *Usanifu wa Maandishi* (94%*) na Fasihi kwa Ujumla* (81.8%)  Pia kiwango cha ufaulu katika mada ya *Riwaya (99.4%) na Maendeleo ya Kiswahili* (99%), kimekuwa sawa kwa miaka yote miwili. Ijapokuwa mwachano wa mada hizi kati ya mwaka 2019 na 2020 ni mkubwa, mada ya *Tamthiliya* imekuwa na mwachano mkubwa zaidi kwani ufaulu wa mwaka 2020 umeshuka kwa asilimia 62.8 ukilinganishwa na ule wa mwaka 2019.

Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika mada karibu zote kwa mwaka 2020 ulikuwa mzuri hivyo, asilimia 100 ya watahiniwa walipata alama zaidi ya 35 katika mada zote. Ufaulu huu ni sawa ikilinganishwa na ufaulu wa watahiniwa kwa mwaka 2019. Watahiniwa wengi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa.

## 5.0 HITIMISHO

Ripoti hii inaonesha kuwa, kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mtihani wa 121 Kiswahili kwa mwaka 2020 kilikuwa kizuri ambapo asilimia 100 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata alama 35 au zaidi. Aidha ufaulu mzuri umetokana na watahiniwa kuwa na maarifa, ujuzi na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa. Kiwango hiki cha ufaulu wa watahiniwa kimekuwa sawa na kile cha mwaka 2019 ambapo watahiniwa walikuwa na ufaulu wa asilimia 100.

Upembuzi yakinifu uliofanyika unaonesha changamoto mbalimbali za watahiniwa wachache walioshindwa kufanya vizuri kama vile: uelewa mdogo wa matakwa ya swali, kujibu kinyume na matakwa ya swali, uelewa mdogo wa mada mbalimbali, uwezo mdogo katika kujibu maswali na kushindwa kutetea hoja walizotoa. Kadhalika, watahiniwa hao walishindwa kutoa mifano dhahiri na ya kutosha katika kujenga hoja za kujibu maswali.

Taarifa hii itawasaidia walimu na wanafunzi kuyaelewa makosa yanayosababisha watahiniwa wachache kutojibu vizuri maswali. Aidha, taarifa hii itakuwa muafaka kwa walimu katika ufundishaji, utungaji na usahihishaji wa mitihani, na hivyo kuinua kiwango zaidi cha ufaulu wa watahiniwa katika somo hili. Pia, ripoti hii italeta hamasa na msukumo chanya wa kujifunza kwa wanafunzi na hasa ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha inayotambulika na kutumika kitaifa na kimataifa ambapo kila mtahiniwa anapaswa awe na uwezo wa kujieleza vizuri, kujiamini na kujivunia lugha hii kama sehemu na utambulisho wa utamaduni wa mtanzania.

## 6.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika mada zilizokuwa na kiwango cha wastani na hafifu, inashauriwa:

(a) Wanafunzi wahimizwe kusoma vitabu vya kiada na ziada ili waweze kupata umahiri na maarifa ya kutosha katika mada za *Usanifu wa Maandishi* na *Tamthiliya*.

(b) Mbinu shirikishi za ufundishaji na ujifunzaji kama vile midahalo, mijadala kwenye vikundi vidogo vidogo na ziara za kimasomo zitumiwe na walimu ili kuwaongezea wanafunzi ujuzi na maarifa katika mada zilizokuwa na kiwango kidogo cha ufaulu (mfano, Usanifu wa Maandishi na Tamthiliya).

(c) Walimu kutumia vielelezo vya kufundishia vinavyoakisi matukio yaliyo katika tamthiliya teule na katika vifungu vya habari/matini za kifasihi.

(d) Walimu kuongoza wanafunzi katika kufanya utafiti/kazimradi ili kubaini mbinu mbalimbali za kifani zilizotumika katika tamthiliya na vifungu vya habari wanavyopewa.

*Kiambatisho A*

**UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2020**

| Na | Mada | Idadi ya maswali | Asilimia ya Watahiniwa waliopata wastani wa 35% ya alama au zaidi | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ufahamu na Ufupisho | 1 | 99.6 | Vizuri |
| 2. | Riwaya | 1 | 99.4 | Vizuri |
| 3. | Maendeleo ya Kiswahili | 2 | 99.0 | Vizuri |
| 4. | Utungaji | 1 | 97.2 | Vizuri |
| 5. | Matumizi ya Sarufi | 2 | 95.8 | Vizuri |
| 6. | Utumizi wa Lugha | 2 | 95.0 | Vizuri |
| 7. | Ushairi | 2 | 86.3 | Vizuri |
| 8. | Fasihi kwa Ujumla | 3 | 70.2 | Vizuri |
| 9. | Tafsiri na Ukalimani | 1 | 69.7 | Vizuri |
| 10. | Usanifu wa Maandishi | 1 | 58 | Wastani |
| 11. | Tamthiliya | 1 | 36.5 | Wastani |

**UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2020**

